
UVCCM wataka mtandao wa X ufungiwe nchini
Uk. 2




EU yaiahidi Tanzania misaada nishati safi
Uk.5



Chadema yadhihirisha wapinzani bado sana!
Uk. 12




Uhuru usiokuwa na mipaka ni wenda-wazimu
Uk. 15



*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo



Makamu wa Rais wa Malawi athibitika kufa ajali ya ndege
Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00069 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Juni 12-18, 2024 |



# Rais Samia acharuka

- Ajifananisha na chura
- Akerwa na wanaotaka kukanyaga uchumi

Lakini katika mageuzi haya tutawakanyaga wengi, wale ambao hawataki kwenda mbele. Na ndiyo watakaopiga kelele nyingi sana...

Uk. 4



## ...Atangaza Siku Maalum ya Gawio kila mwaka

- Mashirika 10 yavuka lengo gawio la chini la bilioni 10/-
- NMB kidedea, yatoa gawio la bil. 54.5/-

## Uvinza waahidi kura za kishindo kwa Samia
Uk. 3

Uk. 2



## Dk. Mwinyi aipongeza taasisi kwa huduma za kijamii

# Dk. Samia atengua RC, DC na kuteua viongozi wanne

**Na Hellen Mwango**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa viongozi na kutengua nafasi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara.

Amemteua aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Momba, Kenan Kihongosi, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu akichukua nafasi ya Dk. Yahaya Nawanda ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Sharifa Nyanga, iliwataja wengine walioteuliwa kuwa ni Elias Mwandobo ambaye anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Momba. Kabla ya uteuzi huo, Mwandobo alikuwa Ofisa Mwandamizi Ofisi ya Rais, Ikulu.

Mwingine ni Christopher Magala, aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu kushika nafasi ya Stephen Mwakajumilo ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Kadhalika, Rais amemteua George Herbet, kuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani. Kabla ya uteuzi huo, Herbet alikuwa Naibu Msaijili wa Mahakama ya Rufani.

Alisema uapisho wa Mkuu wa Mkoa na Msajili wa Mahakama ya Rufani, utatangazwa tarehe itakayopangwa.



# UVCCM wataka mtandao X ufungiwe nchini

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Mohamed Kawaida, ameitaka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuufungia mtandao wa 'X' unaoonyesha maudhui ya ngono yanayokwenda kinyume cha utamaduni wa Watanzania usitumike nchini.

Amesema kwa kuufunga ama kuondoa maudhui yanayohusiana na ngono, utawanusuru vijana wanaoutumia.

"Sisi UVCCM, Jumuiya yetu inafuatilia malezi na makuzi mema ya vijana walioko ndani ya Chama na wasio kwenye chama, haturidhishwi na maudhui ya mtandao huo kwa kuwa yanakwenda kinyume cha maadili ya utamaduni wa Mtanzania," alisema Kawaida alipokuwan akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana na kuongeza:

"Tunaiomba Wizara inayohusika iufungie mara moja au kama wanaweza kuondoa maudhui ya ngono tukaendelea kupata taarifa zenye maadili sawa, lakini kwa ujumla sisi tunachotaka kama haiwezekani, basi kwa Watanzania hatuna kazi nao ufungwe mila zetu haziruhusu."

Aidha, alisema mbali na UVCCM kuyakataa maudhui hayo, pia Serikali na tamaduni za Tanzania, haziruhusu kuangalia maudhui ya ngono kwenye mitandao.

Alisema umefika wakati sasa vijana washikamane kulinda maadili ya kila kijana na wana haki ya kutetea mila na desturi za Tanzania.

"Kuna watu watalalamika, lakini tunasema mtandao huo ufungiwe nchini, ikiwa wizara yetu husika itaweza kuzuia tusione masuala ya ngono, tutaendelea nao, lakini kama itakuwa huru, hatuutaki... Wazungu walituandaa kisaikolojia tukaona 'X' ni neno la kawaida kuna Watanzania zaidi ya 300,000 wanautumia mtandao huu," alisema.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Mohamed Kawaida, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), jijini Dar es Salaam jana.



# Dk. Mwinyi aipongeza taasisi kwa huduma za kijamii

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Taasisi ya Al Mazrui Charitable Organisation ya Abu Dhabi kwa kuendelea kutoa huduma za kijamii ikiwamo huduma za afya, elimu na maji.

Aidha, ameipongeza taasisi hiyo kwa kutoa jengo lake kwa Serikali ili litumike kwa matumizi ya huduma za afya kwa wananchi.

Rais Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na vijana wa Chuo cha Ufundi Mubarak Al Mazrui baada ya kutembelea eneo hilo Mkoa wa Mjini Magharibi jana.

Alisema Serikali imetoa kibali cha kuajiri vijana waliokuwa wanajitolea katika mashirika ya Serikali ikiwemo Mamlaka ya Maji Zanzibar (Zawa).

# Kairuki ateta na Waziri wa Utalii wa Indonesia nchini Hispania

**Na Mwandishi Wetu, Barcelona-Hispania**



WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Utalii na Uchumi wa Jamhuri ya Indonesia, Sandiaga Salahuddin Uno.

Mawaziri hao walikutana na kujadiliana masuala mbalimbali ya ushirikiano katika sekta ya Maliasili na Utalii.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika jijini Barcelona, Hispania, Kairuki alisema kuwa Tanzania iko tayari kushirikiana na Indonesia katika masuala ya utangazaji utalii hasa kwa kutumia njia za kidijitali kimataifa, uhifadhi wa wanyamapori, utoaji huduma kwa wateja na kuvutia mikutano ya kimataifa.

Alitaja maeneo mengine ya ushirikiano kuwa ni mafunzo na kujengeana uwezo akitolea mfano wa mafunzo ya "wellness and spa" na utalii wa matibabu, "Eco tourism," "Green investment" na kuweka mkazo katika matumizi ya nishati mbadala.

Aidha, aliumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji kutoka nchini Indonesia kuwekeza nchini katika huduma ya malazi kwenye maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji ndani ya hifadhi na nje ya maeneo ya hifadhi.

Kwa upande wake, Waziri wa Utalii na Uchumi wa Jamhuri ya Indonesia, Sandiaga Salahuddin Uno, alisema kuwa Indonesia inataka kuimarisha mahusiano baina yake na Tanzania na pia hivi karibuni itakamilisha mchakato wa kusaini Mkataba wa Makubaliano (MOU).

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa, Ali Jabir Mwadini, Mkurugenzi wa Idara ya Utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Thereza Mugobi pamoja na Maafisa Waandamizi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania na Indonesia.

# RC awajia juu mafataki

**Na Allan Kitwe, Tabora**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, amewaonya wanaume wenye tabia ya kulaghai watoto wa shule za msingi na sekondari kwa lengo la kufanya nao mapenzi akisema kiama chao kimefika.

Alitoa onyo hilo hivi karibuni alipokuwa akizungumza na walimu na wanafunzi wa shule za msingi kutoka mikoa 28 ya Tanzania Bara na Visiwani wanaoshiriki Umitashumita mjini hapa.

Alisema serikali imeendelea kuweka mazingira bora katika shule zote ili kuwezesha watoto wote kupata elimu, hivyo, akawaonya wanaume wanaokatisha ndoto za mtoto wa kike.

Alisema atahakikisha watoto wote wa kiume na kike wanalindwa na kupatiwa haki zao za msingi ikiwemo elimu na kuongeza kuwa mafataki wote wanaorubuni watoto wa kike watakiona cha moto.

"Yeyote atakayemchezea mtoto wa kike, kuoa au kumpa mimba, akajisalimishe mwenyewe Kituo cha Polisi hata kabla sijamkamata, katika hili sitapepesa macho, sheria itachukua mkondo wake," alisema.

Alipongeza kazi nzuri inayoendelea kufanywa na serikali katika mkoa huo kwani katika kipindi cha miaka mitatu, wameshapokea zaidi ya Sh bilioni 260 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo katika sekta ya elimu.

Alisema Sh. bilioni 144 zimetumika kuboresha miundombinu ya elimu na michezo, Sh. bilioni 103 zimetumika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari na Sh. bilioni 41 zimegharimia elimu bila malipo.

Aidha, Chacha alimshukuru Rais kwa kuwaletea kiasi cha Sh. bilioni 3.4 kwa ajili ukarabati mkubwa wa shule nne kongwe za mkoa huo ambazo ni Sekondari ya Tabora Wavulana, Tabora Wasichana, Milambo na Kazima.

# Uvinza waahidi kura za kishindo kwa Dk. Samia

**Na Allan Kitwe, Uvinza**

WAKAZI wa vijiji na vitongoji mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma, wameguswa kwa kiwango kikubwa na kasi ya utendaji wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kuahidi kumpa kura za kishindo kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Walibainisha hayo kwa nyakati tofauti walipokuwa wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili ambapo walieleza kufurahishwa na kasi yake ya utekelezaji miradi ya maji katika vijiji na kata mbalimbali ndani ya wilaya hiyo.

Mjasiriamali Uhuru Lubambo (52), mkazi wa Kitongoji cha Kamgumile mjini Uvinza, alimpongeza Rais Dk. Samia kwa kuwapelekea mradi wa maji uliogharimu mamilioni ya fedha na kumaliza kero iliyodumu kwa miaka mingi.

Alisema mradi huo licha ya kuwawezesha kupata huduma ya maji safi na salama ya bomba kwa ajili ya kunywa na matumizi ya nyumbani, pia maji hayo yamemsaidia kustawisha bustani ya miti ya matunda ambayo humpa kipato.

Alisema bustani hiyo imemwezesha kupata zaidi ya Shilingi 400,000 kila mwezi kwa kuuza miti ya matunda na kivuli anayootesha na kumwagilia kwa kutumia maji yaliyoletwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa).

'Tunamshukuru sana Rais Samia kwa kutuletea viongozi wachapa kazi ambao wanasimamia ipasavyo miradi ya maji, kuanzia Waziri mwenye dhamana ya Maji Jumaa Awesu, Mkuu wa Wilaya na Meneja wa Ruwasa wa Wilaya," alisema.

Kwa upande wake, mkulima Stella Kanonko (42), mkazi wa Kijiji cha Kazuramimba, alieleza kuwa miradi ya maji iliyoletwa na Rais Samia, imewapunguzia adha ya kunywa maji machafu na kutembea umbali mrefu kwenda kuchota maji ya mtoni.

"Tunajivunia kuwa na Rais anayejali maisha ya wananchi, tulikuwa tunateseka sana kubeba ndoo za maji kichwani kutoka mtoni au mabondeni, kinamama wa Uvinza tumeshaamua, mwakani tunampa kura zote," alisema.

Mwanachama wa Umoja wa Wanawake (UWT) wa CCM wilayani hapa, Yasinta Ntabirwa, alipongeza kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia ya kutekeleza miradi ya maji mijini na vijijini kwani imesaidia kutatua kero ya maji kwa wananchi.

Alibainisha kuwa wakazi wengi wa mji wa Uvinza walikuwa wanategemea maji ya Mto Luchugi na Malagarasi kwa kunywa, lakini sasa kupitia Ruwasa, wananchi wengi wanapata maji nyumbani kwao au karibu na maeneo yao.

Aliwataka wanawake na wakazi wote wa wilaya hiyo na mkoa mzima, kumuunga mkono Rais Samia atakapochukua fomu ya kugombea urais mwakani ili amalizie miaka yake mitano kwa mafanikio makubwa ya kujivunia.

# RC Makongoro: Wanaotoa huduma za fedha wasajiliwe

**Na Mwandishi Wetu, Sumbawanga**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Makongoro Nyerere, amewataka watoa huduma ndogo ndogo za fedha mkoani hapa, kusajili huduma zao za kifedha kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018 na kutoa elimu kwa wateja wao kabla ya kuwakopesha.

Alitoa maagizo hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana.

"Watoa huduma ndogo za fedha ni watu muhimu katika mkoa wetu na Taifa kwa ujumla. Pamoja na umuhimu huo, naagiza kuwa watoa huduma ndogo ndogo za fedha wote mkoani hapa, wasajiliwe kwa mujibu wa sheria," aliagiza.

Alisema sambamba na zoezi la kusajili vikundi vidogo vidogo vya huduma ndogo za fedha, ni vyema pia kwa watoa mikopo kutoa elimu kwa wanaowakopesha na kuwapa muda wa kuelewa mikataba kabla ya kuwapa mkopo.

"Mtoa huduma za kifedha, toa elimu kwa yule unayetaka kumkopesha kuhusu huduma yako kabla ya kumkopesha. Na hili liende sambamba na wanaokopeshwa kupewa muda wa kutosha kusoma mikataba yao na kuielewa vizuri kabla ya kumkopesha, usimshtukize ule mkataba mpe muda ausome auelewe ndiyo umkopeshe," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa wakuu wa wilaya wote wa mkoani hapa, kuhakikisha kwamba wanasimamia maelekezo yake kuanzia ngazi ya vijiji, kata, tarafa na halmashauri zote.



MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Makongoro Nyerere

# Samia acharuka

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema amejigeuza 'chura' akiwa hasikii wala kujibu kelele nyingi zinazopigwa na watu wanaotaka kukwamisha mageuzi ya kiuchumi anayofanya.

Amesema mtu yeyote anayetaka kumkera, basi amkanyagie uchumi wake.

"Katika mageuzi haya, tutawakanyaga wengi wale ambao hawataki kwenda mbele," alisema.

Alisema hayo katika hafla kupokea gawio na michango kutoka kwa mashirika na taasisi za umma Ikulu jijini Dar es Salaam jana.

Akifafanua hadithi ya chura, Rais Dk. Samia alisema waliwekewa post kwamba atakayefika juu kabisa, atapewa zawadi, sasa chura wakaanza kupanda mmoja mmoja.

Alisema sasa huko chini, watazamaji walikuwa wakiwaambia shukeni mtaanguka shukeni, ninyi hatari hiyo, hamuwezi kufika shuka, mtashindwa tu, basi kelele zikawa nyingi.



Alisema kelele zikawa nyingi kama ambavyo zinazopigwa nchini, hivyo chura wakaanza kushuka mmoja mmoja na akabakia mmoja tu akapanda hadi juu na kuteremka.

"Sasa kama kawaida akazongwa, umewezaje kufika, kumbe yule chura ni kiziwi hasikii, kwa hiyo kelele zote zile alizopigiwa yeye wala, akapanda tu juu na mlingoti wake tu mpaka juu.

"Sasa na mimi nimejigeuza hivyo hivyo chura, nyingi tu zinapigwa kelele. Wakiona hujibu wanasema ngoja sasa tulitukane labda litajibu, sijibu. Najigeuza tu chura, sisikii kabisa. Ninachotaka ni mageuzi ya kiuchumi katika nchi hii na sitaki kingine.

"Sasa kwenye mageuzi haya, tutakanyaga nguru wa Mshihiri. Mnamjua Mshihiri? Mshihiri ni kabila fulani hivi kazi yao ni kuuza nguru. Mnajua nguru? Nguru wale si wanawaanika kwenye jua. Sasa ukitaka kumkera Mshihiri nenda kakanyage nguru wake.

"Kwa hiyo anayetaka kunikera mimi, anikanyagie uchumi wangu. Anikanyagie uchumi wangu.

"Lakini katika mageuzi haya tutawakanyaga wengi, wale ambao hawataki kwenda mbele. Na ndiyo watakaopiga kelele nyingi sana, sasa ndugu yangu wewe, mwanangu wewe uliye kwenye shirika ambaye hutaki kukanyagiwa nguru wako, nenda kachape kazi.

"Leta mageuzi kwenye shirika lako, leta mageuzi, chapa kazi tuone tija inaonekana, inaonekana hivi tija," alisisitiza Rais Dk. Samia.

# ...atangaza Siku Maalum ya Gawio

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametangaza kuwepo kwa siku moja maalum ya kitaifa kila mwaka ambayo Serikali itakuwa ikipokea gawio na michango kutoka kwa mashirika na taasisi za umma.

Alisema hayo katika hafla kupokea gawio na michango kutoka kwa mashirika na taasisi za umma Ikulu jijini Dar es Salaam jana.

"Ofisi yangu ilipokea maombi maalum ya baadhi ya mashirika kutaka kuwasilisha hundi serikalini. Lakini kwa sababu maombi yalikuwa mengi tukikaa kila siku kwa kampuni moja, tukasema aah aah; tukaja na wazo la kuwa na siku hii maalum ya kupokea gawio. Na ni ombi pia la Msajili wa Hazina," alisema.

Mapema akizungumza katika hafla hiyo, Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, alipendekeza kwa Rais Dk. Samia kuwepo kwa siku ya kitaifa ya gawio ambayo itakuwa ikifanyika kila mwaka.

"Ikikupendeza, siku ya leo iwe ya gawio Tanzania, kama itafaa naomba iingie katika ratiba ya ofisi yako kufanyika kila mwisho wa Mei au mwanzoni mwa Juni kila mwaka," alisema na kuongeza:

"Huko makanisani, siku kama hii huitwa Sikukuu ya Mavuno; na kila Ijumaa au Jumapili, kuna sadaka na zaka, sasa serikalini tumesema hebu tuzitafute sana tulete zaka zetu walau mara moja kwa mwaka katika Tanzania Dividend Day."

Akizungumzia ombi la pili alimwomba Rais Dk. Samia kuridhia kuwa mgeni rasmi katika kikao kikuu cha kila mwaka cha wakuu wa mashirika na taasisi za umma pamoja na wenyeviti wao kinachotarajiwa kufanyika wiki ya pili ya Agosti, mwaka huu.

Taasisi 10 zilitoa gawio serikalini katika makundi mawili ambayo kundi la kwanza ni ya mashirika na kibiashara.

Katika kundi hilo liliongozwa na NMB ambayo hundi yake ilikuwa ya Sh. bilioni 54.5 ikifuatiwa na Twiga Minerals iliyotoa hundi ya Sh. bilioni 53.4, Airtel Tanzania Sh. bilioni 40.8, Puma Energy Tanzania Sh. bilioni 12.2, na TPC Moshi Sh. bilioni 10.2.

Kundi lingine ni mashirika yaliyochangia asilimia 15 ya mapato ghafi ambayo ni TPA ilitoa Sh. bilioni 153.9, TCRA Sh. bilioni 34.7, TFS Sh. bilioni 21.3, TASAC Sh. bilioni 19.1 na BRELA Sh. bilioni 18.9.




**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea mfano wa hundi yaSh. bilioni 34.7 kama gawio na michango kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari kwenye hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana.**

# EU yaiahidi Tanzania misaada nishati safi

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Ulaya (EU), umeahidi kuendelea kufadhili miradi ya nishati safi ya kupikia kupitia mfuko maalumu wa nishati safi ili kuiwezesha Serikali ya Tanzania kufikia malengo yake.

Malengo ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2034, asilimia 80 ya Watanzania watumie niashati safi ya kupikia na kuachana na mkaa.

Hayo yalisemwa na Meneja Mradi wa Nishati kutoka EU, Massimiliano Pedretti, kwenye mjadala wa wadau wa sekta ya nishati waliokutana kujadili na kutathmini üelekeo wa sekta ya nishati.

Wadau hao walikuwa wakijadili sekta hiyo ya nishati ilipotoka, ilipo na inapoelekea baada ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 sanjari na changamoto zilizopo na namna ya kukabiliana nazo.

Alisema watafanya hivyo kuunga mkono juhudi za serikali katika mkakati na utekelezaji kufikia azma ya asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Alisema ili Tanzania ifikie azma yake, ni lazima ichukue jitihada za makusudi kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa wauzaji wa mitungi ya gesi, watengenezaji wa majiko ya umeme ili kuchochea wananchi kutumia nishati safi ya kupikia kwa gharama nafuu na upatikanaji wa haraka.

Tayari mradi wa mfuko maalumu wa nishati safi ya kupikia unafanya kazi na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha taasisi kama Magereza, shule, hospitali kupitia Wakala wa Nishati REA, wanafanya kazi kwa pamoja na kuweka miundombinu ya nishati safi ya kupikia kwenye maeneo yao.

Naye Meneja mradi wa matumizi bora ya umeme kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Aaron Cunningham, alisema UNDP iliamua kuunga mkono jitihada za Serikali ya Tanzania kwenye sekta ya nishati safi ya kupikia kwa kuhakikisha pia inaanzisha programu hiyo ili kuwe na matumizi bora ya nishati ya umeme kwenye vifaa vitakavyotumiwa na wadau.



Aliongeza kuwa tayari wameshaainisha viwango vtakavyotumiwa kwenye bidhaa aina tano kama vipoza umeme, jokofu, televisheni, feni na majiko ya umeme ili vitumie umeme kidogo.

Alisema mradi huu unatekelezwa kwa pamoja na Wizara ya Nishati tangu walipoanzisha mwaka 2022 na wamekuwa bega kwa bega na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili viwango hivyo vitoe unafuu wa matumizi ya umeme kwenye vifaa hivyo.

EU imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa kwenye bajeti na miradi ya maendeleo hususani miradi ya umeme.

Nayo Wizara ya Nishati imewatoa hofu wadau wa sekta binafsi kuwa serikali inathamini mchango wa matumizi yote ya nishati safi ya kupikia ikiwemo umeme, gesi na nishati nyingine zote ambazo ni rafiki kwa mazingira na afya.

Hayo yalisemwa kwenye mkutano huo na Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme wa Wizara hiyo, Styden Rwebangila, aliyemwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba kwenye mjadala wa wadau hao wa sekta ya nishati.

''Napenda kuwatoa hofu wadau wa sekta binafsi na Watanzania kuwa nishati safi ya kupikia inajumuusha nishati zote na siyo gesi pekee kama wengine wanavyodhani," alisema Kamishna Rwebangila.

Alisema Wizara ya Nishati inathamini mchango unaotolewa na wadau wa maendeleo hususani EU kwa kufadhili miradi mbalimbali kwenye sekta ya nishati hususani nishati safi ya kupikia na itaendelea kushirikiana nao kwenye upangaji wa mipango mkakati na uendelezaji wa sera.


Mkutano huo uliohudhuriwa na taasisi zilizoko chini ya Wizara ikiwemo REA, EWURA, TPDC, PURA, Tanesco, wadau wa maendeleo na sekta binafsi.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

HII NI KERO

## Jengeni upande huu flyover



Kama kuna sehemu foleni inasumbua sana ni Tazara, hasa kutoka Bandari kuelekea Ubungo. Mara nyingi foleni huanza Kiwanda cha Serengeti na ni eneo ambalo mtu kakaa saa nzima na zaidi kutokana na foleni ni kawaida.

Ingawa upande wa kutoka katikati ya Jiji kwenda Kwanja cha Ndege kuna daraja la juu, lakini serikali ilikosea kuweka daraja hilo sehemu moja na kusahau au kudharau upande wa pili.

Ni wakati mwafaka sasa kujenga daraja la upande wa kutoka badarini kama ilivyo daraja la Ubungo ili kumaliza tatizo hili. Bila shaka hakuna kinachoshindikana Kukiwa na maamuzi na utashi wa kisiasa.



MAONI YA MHARIRI

# Hatuwezi kuendelea kwa kujifungia ndani

Baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kurejea na ujumbe wake wiki iliyopita akitoka ziara ya siku sita nchini Korea Kusini, Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu iliwakutanisha waandishi wa habari na mawaziri waliokuwa kwenye msafara huo kuelezea mafanikio na tathmini ya ziara.

Baadhi ya mambo ambayo mawaziri walisema Tanzania inakwenda kunufaika ni pamoja Wakorea kutusaidia kuboresha viwango vya bidhaa zetu tunazozalisha na kuongezeka maradufu kwa biashara baina yetu na Korea, hususani katika mazao ya kilimo na madini.

Matarajio mengine ni ujenzi wa chuo (atamizi) cha sayansi na teknolojia nchini, kiwanda cha magari cha Hyundai kuunganisha magari yake hapa nchini, kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata madini ya kimkakati hapa nchini, watengeneza filamu wa Tanzania kushirikiana na wa Korea ili kwenda kimataifa na mengine lukuki bila kusahau mikopo ya bei nafuu sana tuliopata.

Lakini lipo hili alilolizungumza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba kuhusu kuwepo kwa Watanzania wanaodhani kwamba safari za nje za viongozi wetu wa kitaifa hazina uhusiano na maendeleo yetu ya ndani. January anasema zina uhusiano mkubwa sana.

Katika dunia ya sasa nchi zinashindana kibiashara na uzalishaji lakini pia zinashirikiana katika mambo mbalimbali kama biashara, kupambana na ugaidi, mabadiliko ya tabianchi, kubadilishana teknolojia na kadhalika na kadhalika

Tunakubaliana na January kwamba huwezi ukajifungia ndani bila kushirikiana na mtu nje halafu ukategemea maendeleo na badala yake hata maendeleo yako ya ndani na matarajio hayatatimia.

Tanzania tunaheshimika huko nje kunatokana na kuwa na misimamo katika masuala ya kimataifa, kauli zetu, tunavyohusiana vizuri na mataifa mengine kisiasa na kiuchumi na hata namna yalivyo maendeleo yetu ya ndani.

Tukumbuke tulijaribu kujifungia na matokeo yake ni kwamba uwekezaji kutoka nje ulipungua sana. Hata kwenye biashara za kimataifa hatukuwa tunafanya vizuri kama tunavyoendelea kufanya sasa na kusema kweli hata heshima ya Tanzania ilipungua. Tuwe wakweli tu.


Lakini pia tunakubaliana na January kwamba, hata kama hatumpendi kwa sababu ya itikadi zetu za kisiasa, hata kama tukiwa hapa ndani tunamchokonoa chokonoa, Samia Suluhu Hassan ndiye nembo ya Tanzania nje ya nchi.

Kwa hiyo anapokuwa nje, ni sura ya Tanzania tutake tusitake, hivyo tuache kuichafua. Tuwe kimya kama hatuna cha kumshauri na akirejea nyumbani basi tuendelee na ukosoaji kama tunao. Hivyo ndivyo mataifa yaliyoendelea na watu waungwana wanavyofanya.

Na hata kwa kiwango cha familia, haipendezi wana ndoa kuanika siri zenu nje badala ya kumaliza kero na tofauti zenu ndani na hasa kwa kuzingatia Rais Samia amefungua milango ya mazungumzo na maridhiano kupitia R zake nne.


## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |

Na Hamid Yassin

JICHO LANGU

# Mizani madukani ikaguliwe mara kwa mara

WATANZANIA hatuoneani huruma hata kidogo kila mtu anaangalia masilahi yake binafsi hata kama anatambua jambo baya analofanya linawaumiza wengine.

Leo nataka kuzungumzia tabia mbaya ya baadhi ya wafanyabiashara kuchezea mizani ya kupimia bidhaa mbalimbali ili kuwapunja walaji kwa maana ya wateja wao ili wapate faida maradufu.

Hili ni jambo ambalo limeota mizizi lakini linachukuliwa 'poa' tu na wahusika huku raia wengi wakiumizwa bila kujua la kufanya.

Nakumbuka ni miaka mingi imepita wafanyabiashara wa maduka ya vyakula ilikuwa ni lazima kila baada ya miaka miwili kupeleka mizani yao kwenye vituo maalumu ili kukaguliwa.

Ilikuwa ni lazima kufanya hivyo kwani baadhi ya wale wenye tamaa ya fedha walishawishika kuzichezea ili uzito usitimie; hivyo wateja wakawa wanapunjwa kwa vitu wanavyopimiwa; udhaifu huo ungali unaendelea hadi leo hii.

Muda si mrefu malalamiko yakawafikia wahusika na wao kwa kweli hawakusita kuyatembelea maduka hayo bila kungoja muda uliopangwa. Walikamatwa wengi wakiwa wameweka vijiwe vidogo ili isigote panapohusika; na kupewa adhabu au kuonywa! Pia adhabu hiyo haikufua dafu! Baadhi waliendelea kufanya biashara hiyo katika mazingira ya kujificha kila kukicha. Pengine wauza nyama na kwenye masoko wanaingiza kwa udanganyifu huu.

> **Nakumbuka ni miaka mingi imepita wafanyabiashara wa maduka ya vyakula ilikuwa ni lazima kila baada ya miaka miwili kupeleka mizani yao kwenye vituo maalumu ili kukaguliwa.**

Cha kushangaza, siku hizi hawa wafanyabiashara wamejisahau kabisa kwamba; mizani yao ni lazima ikaguliwe; na hiyo imetokana na kuwa wale watu wa vipimo hawakagui na kufuatilia ipasavyo kama mizani wanazotumia wafanyabiashara zinafanya kazi inavyopasa au la.

Kwa udhaifu wa viongozi wahusika (Wizara ya Biashara na Viwanda) wafanyabiashara hao wameibuka na mbinu nyingine mpya tena; ambapo huweka mizani yao mahali ambapo si rahisi kuonekana na wateja wakati wa kupima kwa kuiziba na vitu vingine; yaani mizani huonekana sehemu ya juu tu.

Wananchi wanapowalalamikia wafanyabiashara hao, serikali ya mitaa hakuna hatua yoyote inayochukuliwa ila jibu huwa; si la lazima kununua mahitaji yako kwenye duka hilo. Majibu hayo yanatia uchungu kwa wananchi ambao hawajui cha kufanya kwani kwenye serikali ya mtaa hawapati majibu ya kuridhisha.

Zamani maduka hayo yalikuwa yakitembelewa na wakaguzi kutoka wizarani mara kwa mara, mizani hiyo ilikuwa ikikaa mahali pa wazi kwenye maduka yao.

Vitabu vya dini vimekataza wafanyabiashara kipunja wateja kwenye mizani kwamba kiama watakuwa kuni za moto lakini wengi hawajali.

Tunaomba mizani iwe mpya au ya zamani iwe mahali pa wazi ili mteja apate kuona upimaji wa alichokitaka na zikaguliwe. Kama kuna upungufu wa wafanyakazi Wakala ya Vipimo (WMA) waongezwe.

# Vyakula muhimu wanavyopaswa kula watoto kwa afya na ukuaji







KAMA mzazi, mahitaji ya lishe ya mtoto wako mchanga na mtoto aliyekua kidogo, ni wazi kuwa ni kipaumbele na ni rahisi kuhisi kuelemewa na habari nyingi za mitandaoni.

Vyakula ambavyo mtoto hula katika miaka yao ya mapema, vinaweza kuathiri tabia zao za ulaji baadaye maishani.

Kwa hiyo, ni muhimu kuanzisha uhusiano mzuri na chakula tangu umri mdogo na ili kuhakikisha mahitaji ya virutubishi ya mtoto yanatimia, ni muhimu kuzingatia milo mitatu kwa siku. Milo hii inapaswa kujumuisha vyakula kutoka kila moja ya vikundi vitano vikuu vya chakula.

- Vyakula vya protini, kama vile samaki, nyama, mayai na kunde.
- Wanga, kama viazi na wali. Matunda na mboga za rangi tofauti.
- Maziwa na bidhaa za maziwa.

### MIEZI SITA YA MWANZO

Katika miezi sita ya kwanza, maziwa ya mama au maziwa ya unga ya watoto, hutoa nguvu na virutubisho vingi kwa mtoto anavyohitaji hadi kufikia umri wa miezi sita.

Vitamini D ni moja ya virutubisho muhimu. Watoto wanaotumia maziwa ya unga kila siku hawana haja ya kuongeza virutubisho vya vitamin D, lakini watoto wanaonyonyeshwa pekee wanapaswa kupewa virutubisho hivyo.

Serikali ya Uingereza inapendekeza watoto wote wenye umri wa miezi sita hadi miaka mitano wapate nyongeza ya vitamini A, C na D kila siku.

Maziwa ya ng'ombe hayapendekezwi kama kinywaji cha kila siku kwa watoto wachanga kabla ya umri wa mwaka mmoja.

### PROTINI NI MUHIMU KWA MTOTO

Protini ni muhimu kwa ukuaji, ukuaji wa ubongo na kuifanya mifupa imara na yenye nguvu. Vinavyojenga protini ni asidi ya amino, ambayo lazima itoke kwenye chakula. Kuna asidi 20 tofauti za amino, tisa ni muhimu katika lishe ya mtoto.

Protini za wanyama - kama vile nyama, samaki, mayai, maziwa, mtindi na jibini - zina asidi zote tisa muhimu za amino na huchukuliwa kuwa muhimu zaidi kwa ukuaji na maendeleo ya mtoto.

Protini za nafaka, kama vile maharage na kunde, huhesabiwa kuwa ni protini zisizo kamili, kumaanisha zinakosa moja au zaidi ya asidi muhimu ya amino na lazima zitumike na vyanzo vingine vya protini ili kutoa asidi zote zinazohitajika.

Serikali ya Uingereza inapendekeza kula samaki mara mbili kwa wiki, ikiwa ni pamoja na samaki wenye mafuta.

Mazao ya mashambani au yaliyosindikwa ni mazuri, lakini kumbuka kuwa mazao yaliyokaushwa na ya makopo, huwa na chumvi nyingi.

### WANGA KWA MTOTO

Vyakula vya wanga ni muhimu kwa sababu ni chanzo muhimu cha nishati ya mwili na hutoa nyuzi nzuri kwa usagaji chakula.

Watoto wanahitaji wanga katika kila mlo - mkate, viazi, wali. Hata hivyo, watoto wadogo (hasa wale walio chini ya umri wa miaka miwili), wanaweza kupata ugumu wa kusaga aina za nafaka na nyuzinyuzi zinaweza kuwafanya wajisikie kushiba haraka, hivyo kuhatarisha hamu yao ya kula.

Kidogo kidogo, watoto wapewe wanga wenye nyuzi ili mfumo wa Usagaji chakula wa mtoto wako uweze kukabiliana na nyuzinyuzi za wanga.

Vyakula vya wanga ni muhimu kwa sababu ni chanzo muhimu cha nguvu na hutoa nyuzi ambazo ni nzuri kwa usagaji chakula.

### MATUNDA NA MBOGA KWA MTOTO

Matunda na mboga, hutoa vitamini, madini na nyuzi. Inashauriwa kuanza kuwapa watoto baada ya umri wa miezi sita.

Saizi ya kutumikia inategemea umri, urefu na shughuli za mwili za mtoto, kwa hivyo hakuna sheria zilizowekwa. Njia rahisi ni kumpa kiasi ambacho kinafaa kwenye kiganja cha mkono wa mtoto.

>>>Inaendelea Uk. 8

> Protini za nafaka, kama vile maharage na kunde, huhesabiwa kuwa ni protini zisizo kamili, kumaanisha zinakosa moja au zaidi ya asidi muhimu ya amino na lazima zitumike na vyanzo vingine vya protini ili kutoa asidi zote zinazohitajika.



# Vyakula muhimu wanavyopaswa kula watoto kwa afya na ukuaji



> Unapomnyonyesha mtoto, ni vyema kuendelea kumnyonyesha, ikiwa unaweza, ambayo itasaidia lishe yake wakati wa kumpa aina nyingine za chakula.

>>>Inatoka Uk. 7

Matunda yaliyokaushwa yanapaswa kupewa watoto pamoja na mlo mwingine badala ya kumpa kama yalivyo, kwani kiwango cha juu cha sukari kinaweza kusababisha kuoza kwa meno.

**VIPI KUHUSU MAZIWA?**

Unapomnyonyesha mtoto, ni vyema kuendelea kumnyonyesha, ikiwa unaweza, ambayo itasaidia lishe yake wakati wa kumpa aina nyingine za chakula.

Maziwa yote na bidhaa za maziwa (ikiwa ni pamoja na maziwa, mtindi na jibini), ni chanzo muhimu cha kalsiamu na iodini, pamoja na vitamini A, D na B12.

Baada ya umri wa mwaka mmoja, unaweza kumpa maziwa ya ng'ombe na inashauriwa kumpa maziwa mara mbili kila siku kama vile maziwa, jibini, mtindi au jibini.

Kwa watoto wenye umri wa mwaka moja hadi miwili, chagua maziwa yoyote, kwani ni muhimu kwa ukuaji na kupata vitamin muhimu.

Zaidi ya hayo, maziwa yenye mafuta kidogo, huenda yasitoe kalori au vitamini zinazohitaji. Unaweza kumpa maziwa yenye mafuta, ilimradi tu mtoto anakula aina mbalimbali za vyakula na kupata uzito kawaida.



Bidhaa na maziwa zenye mafuta kidogo zina kalsiamu nyingi kama yale yaliyo na mafuta mengi, lakini maziwa yenye mafuta kidogo, yanapaswa kuepukwa hadi mtoto atakapofikisha umri wa miaka mitano.

Inafaa kukumbuka kuwa mtindi wa viwandani mara nyingi hupakiwa na sukari, hivyo epuka mtindi wenye ladha. Badala yake, chagua mtindi wa asili.

**MAFUTA NA SUKARI KWA MTOTO**

Ingawa watoto wanahitaji kiasi fulani cha mafuta ili kukua, haipendekezi kumpa kiasi kikubwa cha mafuta ya aina yoyote.

Siagi ni chanzo cha nishati ya mwili, muhimu kwa watoto wadogo ambao wanakua haraka na wanafanya kazi za kimwili.

Mafuta pia ni muhimu ili kuwezesha ngozi kupata vitamini fulani, ikiwa ni pamoja na vitamini A, D, E na K. Ni muhimu kwa kazi ya kinga na utendaji wa ubongo.

Mafuta yanapatikana katika samaki, karanga, mbegu na mafuta yao. Hata hivyo, karanga nzima na mbegu, zinapaswa kuepukwa hadi mtoto awe na umri wa miaka mitano kutokana na hatari ya kupaliwa.

Vinywaji laini, pipi, biskuti na keki - mara nyingi huwa na sukari nyingi. Ulaji wa vyakula vilivyoongezwa sukari, mafuta na chumvi nyingi kupita kiasi, ni mojawapo ya sababu kuu zinazochangia unene wa kupindukia.

**VITAFUNIO KWA MTOTO**

Ni muhimu kwa mtoto mdogo kula vitafunio vinavyofaa (siyo kula mara kwa mara) ili kudumisha hamu yao ya kula.

Kadiri unavyomsaidia mtoto kujua wakati wa kula, ndivyo atakavyoamua ni chakula gani anachopaswa kula anapokua.

Watoto wanapoomba chakula, hakikisha kuwa hana kiu, kwani wakati mwingine huchanganyikiwa.

Matunda kama zabibu, ni chaguo zuri kwa watoto. Vilevile, kutafuna vitu kama karoti, tango au nyanya, pia ni chaguo nzuri.

Juisi inaweza kuwa njia nzuri ya kuhimiza watoto kuongeza ulaji wao wa vitamini C, kwa mfumo wao wa kinga, uzalishaji wa nishati na kuzuia upungufu wa damu.

Lakini kula matunda bora kwa watoto (na meno yao) kuliko juisi hasa zinazoongezwa sukari, ambayo ni vyema kupunguza kutumia. Kinachofaa zaidi ni kuyafanya maji kuwa kinywaji kikuu cha mtoto na asizidishe glasi moja ndogo ya juisi.BBC.





*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Juni 12-18, 2024 |

JAMII
UCHUMI
SIASA

Jarida hili haliuzwi

# Chadema yadhihirisha wapinzani bado sana!

UK. 12 & 13





# Madhara ya mabadiliko ya tabianchi nani alaumiwe?

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Mwenyezi Mungu aliye Alfa na Omega; aliumba Dunia pamoja na vyote vijijazavyo . Kulingana na Maandiko Matakatifu, Mungu alisiimika dunia katika misingi yake kwa uhakika na weledi mkubwa.

Maandiko pia yanatuhakikishia kuwa vyote Mungu alivyoviumba, iwe vilivyopo juu angani; kwenye uso wa dunia na chini ya ardhi, baharini na vyote vilivyomo; alivikamilisha katika muda wa siku tano tu na siku ya sita akakamilisha kazi ya uumbaji kwa kumuumba binadamu na siku ya saba Mungu akapumzika baada ya kuona vyote alivyoumba viko katika usitahili wake na kupendeza. Mungu akavibariki vyote alivyoviumba na kuvipa uwezo wa kuongezeka na kujaza anga zima juu, vilivyo chini ya ardhi, pamoja na kwenye maji katika mito, maziwa, mabwawa na baharini. Vilevile, Mungu akaweka jua (nuru, wakati wa mchana) na giza (wakati wa usiku) hivyo ikawa mwanzo wa kuwepo majira, misimu na nyakati tofautitofauti.

Sasa ni mamilioni ya miaka mingi sana yamepita tangu kazi ya uumbaji ifanyike na Mungu akakasimu kwetu wanadamu madaraka kamili ya kuvimiliki na kuvitawala viumbe vyote.

Je, katika kulitimiza jukumu hilo la kumiliki na kutawala, hadi kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kupelekea mabadiliko makubwa ya tabianchi, nani aliyezembea, anayestahili kulaumiwa? Je, ni wanadamu wa kwanza Adam na Eva (Hawa) au vizazi vilivyofuata au nini chimbuko la hayo yote kiasi kwamba kizazi cha sasa kinahaha kwa mahangaiko makubwa kutokana na halihalisi iliyojitokeza kuhusu uharibifu wa mazingira na madhara makubwa yatokanayo na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi?

Uzoefu tulionao unatuonyesha kuwa inapotokea changamoto kubwa tunasema asitafutwe mchawi bali tugange yaliyotokea . Wakati mwingine unasikia tusifukue makaburi maana tutapelekea ukosefu wa amani au kusababisha maumivu makali kwa baadhi ya wahusika au utajenga uhasama bila kutarajia .

Je, kwa hali hii ya mabadiliko ya tabianchi, wakati baadhi ya mataifa yanateseka kutokana na uchafuzi mkubwa wa mazingira wakati huo mataifa machache yakipeta huku tukijua wao ndiyo chimbuko kubwa la uharibifu mkubwa wa mazingira, tutaendelea na hali hiyo hadi lini?

Kwa upande wa taifa letu pia tujichunguze ili tufahamu sawasawa hali halisi ilivyo kwenye mazingira yanayotuzunguka, tangu tulipoanza kutawaliwa na wakoloni miaka ya 1880 hadi sasa. Je, hali ya mazingira kwenye maeneo mbalimbali nchini ilikuwa ikoje tukilinganisha na hali ya sasa?

Kufanya tathmini kama hiyo ni muhimu ili kujua tumejikwaa wapi. Tujitathimini hali ya mazingira ilikuwaje nyakati hizo za ukoloni na baada ya kujitawala hadi sasa kumekuwepo na mwelekeo gani na je, tunaelekea wapi kwa miaka ijayo?

Watawala wa kikoloni waligundua kuwa shughuli za kibinadamu ambazo zilikuwa siyo endelevu zinasababisha kutoweka kwa misitu ya asili kwa haraka kutokana na kilimo cha kuhamahama na kuchoma moto mapori hovyo vyakati za kiangazi.

Jitihada zao za kupambana na hali hiyo hazikusaidia kutokana na uwezo mdogo waliokuwa nao wakati huo. Hata hivyo, waliona vyema, baadhi ya maeneo yenye misitu iliyofaa kuhifadhi mazingira, bioanuwai (biodiversity) ikiwemo vyanzo vya maji; ikatengenezewa sheria ya kulinda misitu iliyohifadhaiwa.

Katika kuitekeleza sheria, misitu husika ikawekewa mipaka rasimi na kutengeneza ramani. Vilevile, ikagawanywa kwenye maeneo ya kuisimamia (Ranges), kuwekewa walinzi misitu (Forest Rangers) na kuandaliwa mipango ya kuisimamia.

Baada ya hatua hiyo, hakuna mtu aliyekuwa anaruhusiwa kufanya shughuli yoyote katika misitu iliyohifadhiwa bila kibali maalumu.

Hao walikuwa Wajerumani na baada ya Waigereza kuchukua madaraka wakati Vita ya Kwanza ya Dunia kumalizika mwaka 1918; waliendeleza kasi ya kuyahifadhi baadhi ya maeneo yenye misitu sitahili na kuyawekea walinzi misitu. Kwa ujumla, misitu zaidi ya 250 yenye hadhi ya kuhifadhiwa ikahifadhiwa kati ya 1990 na 1961.

Tulipojitawala tukaendeleza juhudi hizo hadi tukafikia misitu zaidi ya 600 chini ya Serikali Kuu na takribani misitu iliyohifadhiwa 200 ikawa chini ya usimamizi wa halmashauri za wilaya.

Wakati wa kuyafanya hayo, juhudi za kuzuia uharibifu wa misitu kwenye maeneo ya vijiji, kutokana na kilimo cha kuhamahama pamoja na kuchunga mifugo kiholela, hazikuwa za kutosha hivyo, uharibifu uliendelea.

Pamoja na kwamba wakoloni walianzisha Chuo cha Misitu kwa Wataalamu wa Kati (technical cadre) Olmotonyi, Arusha kati ya 1937 na 1938; hakikuwa na uwezo wa kutoa wataalamu toshelezi.

Kati ya mwaka 1970 na 1974 mafunzo ya misitu kwa ngazi ya shahada yalianzishwa Morogoro katika Kitivo cha Kilimo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hivyo kuwezesha taifa kuwapata wataalamu husika (professional cadre).

Wakati huohuo, Serikali ilikuwa na mkakati wa kuokoa maeneo yaliyokuwa yameheribiwa na mimomonyoko ya udongo hivyo kusababisha makorongo makubwa katika Mkoa wa Dodoma (HADO) hususani eneo la Haubi, Kondoa Irangi, Wilayani Kondoa pia kuanzisha mradi Mkoani Shinyanga wa Hifadhi Ardhi Shinyanga (HASHI) pamoja na kuokoa maeneo kadhaa katika mikoa ya Arusha (sehemu za Babati) na Iringa (Isimani) yalishughulikiwa kwa misaada ya wahisani kutoka nje ya nchi.

Hata hivyo, juhudi za kuilinda na kuisimamia misitu ya asili Tanzania Bara, zilianza kupungua nguvu baada ya watunga sera/wafanya maamuzi kupitisha sera iliyopelekea dekta fulani kupewa kipaumbele cha kitaifa kuliko nyingine.

Hali hiyo ikapunguza bajeti iliyokuwa inatengwa kwa ajili ya kuisimamia na kuitunza misitu. Ikafika mahali, hata Kada ya walinzi misitu iliyoanzishwa wakati wa wakaoloni ikafutwa. Kitendo hicho kikapelekea juhudi za kuisimamia na kuilinda misitu kuzorota.

Hali hiyo pamoja na kukosekana kwa matumizi bora ya ardhi, ongezeko la namba ya watu na mifugo bila kusahau matumizi makubwa ya mkaa ; kuchoma moto mapori hovyo, kila mwaka; yote hayo yakasababisha maumivu makubwa kwenye misitu ya asili.

Kilichoendelea baada ya hapo, uwezo wa Idara kuisimamia misitu ukapungua (watumishi wachache na uhaba ya vitendea kazi) hivyo, kidogokidogo, misitu ikawa inapoteza uhalisia wake kila mwaka. Kadhalika, kasi ya mimomonyoko ya udongo, ikawa inaongezeka hivyo, uharibifu wa mazingira kuonekana kitu cha kawaida vijijini na mijini (uchafu, vitendo vya kutupa taka hovyo kushamiri).

Kimataifa, hasa kwenye nchi zilizoendelea mathalani, Marekani na nchi za Ulaya; matumizi ya nishati inayozalisha gesiukaa (kaboni) kwa wingi katika viwanda hivyo kumepelekea ongezeko la joto duniani.

Tangu 1992 hadi sasa, kupitia Umoja wa Mataifa, pia kumekuwa kukifanyika mikutano kila mwaka, kutafuta maafikiano kuhusu nini kifanyike ili kuzuia ongezeko la joto duniani. Mkutano wa kwanza ulifanyikia Rio De Janeiro, Brazil na Tanzania ilishiriki kikamilifu na hata sasa tunahudhuria vikao vya kimataifa tukitarajia kupata suluhisho la kudumu juu ya ongezeko la joto linalochangia pakubwa mabadiliko ya tabianchi (climate change).

Tangu 1992 hadi sasa ni takribani miaka 32 lakini maafa yanazidi kushamiri kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Mtoto aliyezaliwa mwaka huo amekua, akasoma hadi chuo kikuu na kufanikiwa kupata digrii mbili/tatu mataifa bila kufanikisha lengo la kuzuia joto lisizidi digrii mbili (2oC) Celsius, kwa viwango vya miaka 1990.

Najiuliza, tunakwama wapi au ndiyo michakato ya kidiplomasia inavyokuwa (hakuna kulazimishana) hadi matajiri waone wameguswa kwa kiasi kikubwa ndipo wachukue tahadhari?

Waswahili husema kuchukua tahadhari mapema ni bora zaidi kuliko kuhangaika na madhara hasi au heri nusu shari kuliko shari kamili .

Kwa hali ya sasa duniani ilivyo, Watanzania tuchukue maamuzi magumu, mapema kuhakikisha tunalinda mazingira ili kujinusuru na madhara yasiyotarajiwa. Tusingoje hadi hali imekuwa hatarishi kwa maisha yetu na viumbe wengine ndipo tuhangaike kufanya marekebeshisho maana gharama zake ni kubwa sana.

***[Makala itakayofuata itajikita kwenye Nini kifanyike ili kuyanusuru mazingira yasendelee kuharibika na kuhatarisha uhai nchini].***



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Tukumbushane jambo hili muhimu kuelekea chaguzi zetu

"Bila shaka miongoni mwenu wamo ambao wanataka kuingia kwenye uwanja wa siasa; lakini swali la msingi ni kwa nini unataka kuongoza? Barani Afrika, njia rahisi ya kujipatia utajiri kwa njia zisizo halali ni uongozi wa kisiasa. Unapata utajiri ambao haukuutolea jasho kabisa," anasema Profesa wa sheria, mwanaharakati na mchambuzi mahiri wa masuala mbalimbali kutoka nchini Kenya, Profesa Patrick Lumumba.

Lumumba, katika hotuba niliyomkariri akisema maneno hayo, alizidi kusema: "Kwa bahati mbaya sana, wapiga kura nao wanakumbatia jambo hili ovu... Nao wanatarajia kuhongwa na wagombea ili wawapige kura."

Kisha mwanamajumui hiyo akasema: "Mpaka pale tutakapotatua tatizo la ubaguzi (kumchagua mtu kwa kabila, dini, umajimbo, uswahiba) na rushwa, Afrika haiwezi kupata viongozi wazuri."

Maneno haya ya Profesa Lumumba, yanakaribiana na yale aliyoyasema Mwalimu Nyerere enzi za uhai wake wakati tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 1995. Mwalimu alisema kwamba rushwa kwenye siasa ni ufa hatari unaotakiwa kuzibwa.

"Uchaguzi wa mwaka huu (1995) utakuwa ni uchaguzi wa pesa. Zamani katika CCM na katika Tanu, tunapochagua candidate (mgombea) wetu, kama ana mali tunamuuliza, hii mali umepata wapi? Mali ilikuwa disqualification (kigezo cha kutochaguliwa kugombea). Mwaka huu (1995), mali itakuwa number one qualification (kigezo cha kwanza kuchaguliwa), wamezipata wapi? Huo tunadhani ni ufa wa tatu. Ulitikisa na umetikisa."

Profesa Lumumba pia alipata kusema kwamba kimsingi katika chaguzi zetu, wapiga kura wa Afrika ni kama vile tunapewa hundi ili kuandika kiasi wanachotaka (blank cheque) kwa maana ya kupewa nafasi ya kuchagua kiongozi atakayetupa maendeleo. Lakini ajabu tunashindwa kutumia nafasi hiyo adhimu kuchagua viongozi watakaotutumikia na badala yake tunachagua viongozi watakaojiwakilisha wenyewe na matumbo yao!

Profesa Lumumba huwa anasema kuchagua kiongozi kwa sababu amekuhonga fedha au kwa sababu ni kabila au dini yako bila kuangalia maono na uwezo wake katika uongozi basi usitegemee atajikita katika kushughulikia kero zako kwa dhati kabisa kabisa.

Kwa msemo wa Profesa, ni sawa na kununua pikipiki halafu utegemee ije ifanye kazi kama Benzi. Sahau!

Prof. Lumumba amekuwa akisema bila kutafuna maneno kwamba janga kubwa la Afrika ni watu kuchagua viongozi wezi kuanzia ngazi za mitaa hadi ngazi za juu huku watu safi katika jamii wakipuuzwa.

Juni 3 mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene aliwataka viongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutumia taaluma na ujuzi walio nao katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kupokea rushwa hasa katika kipindi cha uchaguzi wa viongozi mbalimbali.

Simbachawene alitoa agizo hilo katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha mkoani Pwani wakati akifungua kikao kazi cha viongozi wa Takukuru kilicholenga kujiimarisha zaidi katika kuzuia na kupambana na rushwa wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Waziri huyo anasema ni wakati sasa wa wananchi kupewa elimu kwa nguvu zote juu ya rushwa katika chaguzi ili kupata viongozi bora kwa maendeleo ya taifa kwani kuna kundi kubwa la wananchi linaamini kuwa wakati chaguzi ni wakati wa mavuno kwao, kwa maana anayetaka kugombea naye awape rushwa ili wampigie kura. Huu ni msiba!

"Kuzuia wanaotaka kutoa rushwa pekee hakutoshi kwani makundi ya wapiga kura wanasadiki kuwa mtu hawezi kumchagua kiongozi anayemtaka mpaka awe amepewa chochote, hivyo tuwaelimishe na tuyaishi maisha ya kwenye vitabu vya dini kuwa anayetoa na anayepokea rushwa, wote wana hatia," anasema.

**Kuzuia wanaotaka kutoa rushwa pekee hakutoshi kwani makundi ya wapiga kura wanasadiki kuwa mtu hawezi kumchagua kiongozi anayemtaka mpaka awe amepewa chochote, hivyo tuwaelimishe na tuyaishi maisha ya kwenye vitabu vya dini kuwa anayetoa na anayepokea rushwa, wote wana hatia.**

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Salum Hamduni alisema watajipanga vema ili kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa ufanisi mkubwa bila ya kuwa na chembechembe za rushwa ili kuwapata viongozi bora kwa maendeleo ya taifa.

Maelezo hayo ya bosi wa Takukuru ni ya msingi lakini elimu kwa Watanzania kuelewa madhara ya kununua pikipiki na kudhani itawafanyia kazi kama Benzi ni muhimu zaidi. Kama wananchi hawatakuwa tayari kupokea rushwa, hakutakuwa na wa kumpa rushwa na wakaoingia kichwakichwa itakuwa rahisi kuwadaka pia.

Mafundisho ya dini ya Kiislamu yanaonesha kwamba kati ya watu watakaokuwa na msalaba hatari Siku ya Kiama ni viongozi wasio waadilifu.

Baada ya Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) kuondoka duniani, tunajifunza kwamba kila swahaba (mwanafunzi/mfuasi wa Mtume) aliogopa kujitokeza kichwakichwa kuchukua hatamu za kuongoza waumini. Walichokuwa wanaogopa ni hofu kila wakijiuliza kama watatenda uadilifu ipasavyo. Walijiuliza, je, wataingia kiburi na kupandisha mabega? Watatenda haki kwa kila mtu? Hii ni kwa sababu walijua na kuwa na uhakika kwamba kuna siku watasimama kwenye mahakama tukufu ya Mwenyezi Mungu. Je, watajibu nini wakivurunda?

Tunasoma kwenye historia (sirra) kwamba kiongozi wa kwanza wa waumini (kwa mujibu wa mafundisho hayo) alikuwa Abubakar Sadiiq, lakini hadi kukubali uongozi alifuatwa mara kadhaa na maswahaba wenzake wakisema kwa jinsi wanavyomwona na jinsi alivyomwadilifu anafaa achukue haramu za uongozi. Yeye alijitahidi sana kukataa akihofu kubeba mzigo hatari mwishoni akakubali. Ndivyo pia ilikuwa kwa viongozi wengine waliofuatia.

Ninaandika haya nikijua viongozi wengi wa dini hiyo wa sasa dunia imewakamata kiasi kwamba hawaogopi na wanakimbilia madaraka na hasa kama kuna maslahi fulani ya kidunia! Hili si la kuficha. Naamini wanajua kwamba madaraka wanayokimbilia ni 'mtego' hatari kama wanavyosema vijana kwani kama hawatafanya uadilifu, moto unawasubiri!

Mwalimu Nyerere alipata kusema pia maneno takribani sawa kabisa na mafundisho haya ya Uislamu. Alisema maneno haya. "Ikulu ni mahala patakatifu. Mtu safi kabisa kabisa hawezi kupakimbilia... Utaoni watu wanaumwa, wana kero na matatizo haya na yale basi ujue huo ni mzigo wako."

Ingawa Mwalimu alilenga uongozi wa juu wa nchi yetu alipotamka Ikulu, lakini hilo linamgusa kila kiongozi kuanzia familia, mjumbe wa mtaa, diwani, meneja wa kampuni, mkurugenzi, mbunge na kadhalika.

Ukiwa diwani, kwa mfano, wewe ni mwakilishi wa wananchi wa eneo lako kwenye halmashauri. Kero za wananchi ambazo zinaweza kutatuliwa katika ngazi ya halmashauri, usipozitafutia ufumbuzi wakati ni mzigo wako, wewe si mwadilifu na siku ya Kiama ni haki kabisa utupwe motoni!

Mwalimu alisema mtu wa kuogopwa kama ukoma ni yule anayepita kuomba kuchaguliwa huku akitoa rushwa na ndipo akahoji; Hizi fedha atazirudishaje?

Jibu ni kama tulivyoanza andiko hili pale Profesa Lumumba anaposema kwamba Barani Afrika, njia rahisi ya kujipatia utajiri kwa njia zisizo halali ni uongozi wa kisiasa! Hivyo mtu huyu anachotafuta si kutatua kero za wananchi bali kutatua shida zake kupitia kodi zetu!

Kwa maneno mafupi sana, ninachosema hapa ndugu zangu ni kwamba Takukuru, viongozi wetu na taasisi nyingine zakiwemo za kidini, wana dhima kubwa ya kuwazindua Watanzania kujitambua kuhusu kosa kubwa la kuendekeza njaa na kuchagua viongozi watoa rushwa.

Ninawashauri wahusika wakiwemo Takukuru kutumia waandishi wa habari na wasanii kufikisha ujumbe kama huu kwa Watanzania tunapoelekea kwenye chaguzi zilizo mbele yetu. Si vibaya wakawa na bajeti kwa ajili hiyo.

Na kwa wananchi wenzangu, mnaonaje tukianza kwenye mitaa yetu kusaka watu tutakaowachagua kwenye serikali za mitaa/vijiji, diwani hadi mbunge baada ya kujiridhisha kwamba ni waadilifu, wana maono na wanaweza kusaidia jamii. Tusisubiri waje kutuomba, bali sisi ndio tutoke tukawaombe wagombee baada ya kuona wanatosha.

Ikiwezekana tujichangishe wenyewe kugharimia kampeni zao kwa sababu tunataka watufanyie kazi sisi za kupeleka kero zetu kwenye vyombo vya maamuzi. Naamini siku tukifanya hivi tutapata wawakilishi/viongozi wa kweli ambao watatutumikia sisi na si vinginevyo.

# Chadema yadhihirisha wapinzani bado sana!

Na Hamid Yassin

KULIPUANA hadharani kunakoendelea miongoni mwa viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kunadhihirisha kitu kimoja kikubwa; kwamba wapinzani bado hawajaiva kukabidhiwa mamlaka ya kuongoza taifa hili.

Katika kipindi hiki cha uchaguzi wa ndani wa Chadema ambacho kinachukuliwa kama chama kikuu cha upinzani tumesikia na kushuhudia madudu mengi ambayo ni dhahiri yanabainisha kwamba hakistahili kuaminika mbele ya Watanzania kwani bado kinakosa sifa ya uongozi,

kama viongozi wakuu wa chama wanatukanana hadharani, wanachafuana mchana kweupe kisa, matabaka ya viongozi kwenye chaguzi za ndani ya chama; Je, tukiwakabidhi nchi itakuwaje? Si watatuuza hawa asubuhi tu!

## WAELEKEZANA MAKOMBORA

Yale maneno ya makombora makali waliyokuwa wakiwatupia viongozi wa chama tawala CCM, hivi sasa wameyaelekeza kwenye ngome yao na wanajilipua wenyewe kwa wenyewe!

Tulikuwa tunaambiwa CCM kuna mafisadi papa, kumbe Chadema wamejaa tele na walikuwa wanatuficha ili tuwakabidhi nchi 'waishughulikie' barabara! Sasa Mwenyezi Mungu amewalaani wameanza kutafunana wenyewe kwa wenyewe kama wachawi!

Kimsingi, ukisoma ule waraka wa Mkakati wa Mabadiliko uliosababisha akina Zitto Kabwe wakafukuzwa Chadema, ukiusoma katika mistari utagundua kwa Chadema kuna ufisadi lakini sasa mambo yanazidi kuwa hadharani.

Bila shaka Watanzania wanakumbuka ngebe za viongozi wa vyama vya upinzani zilizokuwa zikidai kuwa Serikali za CCM tangu ya hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi mpaka ile ya awamu ya tano ya hayati John Pombe Magufuli zilikuwa za kifisadi na zisizoleta maendeleo yoyote.

Kibaya zaidi ni pale walipokwenda mbali mno kwa kudai kuwa baadhi ya awamu kwenye hizo serikali chini ya Chama Cha Mapinduzi zilikuwa na viongozi legelege na wasioweza kwenda na kasi ya mapambano ya ufisadi na uhujumu wa mali ya umma.

Kana kwamba hiyo haitoshi, wapinzani hao walithubutu kumtusi aliyekuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Awamu ya Nne, marehemu Edward Ngoyai Lowassa kwa kumtangaza kuwa alikuwa fisadi nambari moja kati ya 20 waliowaita kwa lugha ya Kiingereza "List of Shame" kwa maana ya "Orodha ya aibu".

Kwa maana kubwa zaidi ni kwamba orodha ile ilikuwa ya watu wa hovyo kupita kitu chochote kile kutokana na ukweli kwamba walituambia ilisheheni wahujumu uchumi wa Taifa hili na hawakustahili kukabidhiwa dhamana ya kuongoza nchi hii!

Achilia mbali chaguzi za mwanzo za mfumo huu wa vyama vingi, kwenye kampeni za mwaka 2015 za kwenda Ikulu, pamoja na wapinzani kumuunga mkono hata kwa unafiki tu, bali walikaa kimya muda wote huku kama kawaida wakitafuta makosa ili kumsema vibaya!

## UFISADI NA HILA

Kabla hatujasahau yale 'mabomu' yao ya mafisadi papa ndani ya CCM, sasa wameamua kuweka wazi kwamba si lazima chama kishike dola ndiyo kiwe na mafisadi bali hata huko upinzani wamejaa kama wote!

Si maneno yangu haya, bali mlengwa mkubwa akiwa Bosi wake Mbowe.

Wakati tunamshangaa Lissu ambaye ndiye alikuwa kinara kudai CCM ina Mafisadi Papa, sasa ameibuka aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Utendaji wa chama hicho kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Simon Msigwa na kunena yaleyale ya Makamu Mwenyekiti kwamba uchaguzi huo umejaa rushwa na hila kibao!

Mchungaji Msigwa Mabadiliko 2013 kwa kuugoogle kwenye mtandao.

Mchungaji anasema rafu alizochezewa si za nchi hii! Anamtaja Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Bara, Benson Kigaila aliyetumwa na Makao Makuu kwenda kusimamia uchaguzi huo wa Kanda ya Nyasa kwamba, alikwenda kule akiwa na maelekezo maalumu ya kuhakikisha hashindi uchaguzi huo!

Anadai licha kuibiwa kura mchana kweupe, lakini



Peter Msigwa

hao kuwataka wananchi wasiichagure CCM kurejea Ikulu, lakini waliendelea pia kudai kuwa chama hicho hakina jipya katika kuongoza nchi hii.

Cha kushangaza ni kwamba wapinzani haohao walikuwa wakitupa makombora hayo huku wakiwa na mtu ambaye wao wenyewe walimwita fisadi nambari moja akiwa ndio Rais wao mtarajiwa, hayati Lowassa!

Ukweli kwamba Chadema hii si chama cha kupambana na ufisadi kama walivyokuwa wakitudanganya ulianza kujitokeza pale Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli alipoanza kutumbua mafisadi, lakini hawakuonesha kabisa ni ya viongozi waandamizi wa Chadema ambao wametudhihirishia kwamba ndani ya uchaguzi wao wa ndani unaoendelea nchini kote kuna ufisadi mkubwa, wizi na hila kibao!

Alianza Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu akifichua kwamba Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe ana genge lake analotaka lishike hatamu ya kuongoza chama hicho na analiwezesha fedha za chama chao kinyemela.

Lissu ameweka wazi kwamba chaguzi za ndani zinaoendelea ndani ya chama chao zimegubikwa na rushwa na ufisadi uliokithiri huku aliyebwagwa na Joseph Mbilinyi 'Sugu' kwenye uchaguzi huo wa Kanda ya Nyasa kwa kupata kura 52 dhidi ya 54, anadai uongozi wa juu wa chama hicho kambi ya Mwenyekiti wao Mbowe ulituma wasimamizi maalumu wa uchaguzi huo kule Nyanda za Juu kwenda kumuangamiza yeye!

Kiongozi huyu aliyeshika wadhifa wa uenyekiti wa Kanda hiyo kwa vipindi vitatu, anasema Mbowe anatengeneza safu yake ya uongozi ndani ya Chadema ili aendelee kukiburuza chama hicho milele!

Sauti kama hii unaweza kuisikia vizuri zaidi ukisoma Waraka wa Mkakati wa wapigakura watatu waliokuwa upande wake walizuiwa kupiga kura kwa masilahi ya mpinzani wake, Mr 'Sugu'.

## HATA CCM WANATOFAUTIANA

Kutofautiana miongoni mwa binadamu hususani viongozi, ni jambo la kawaida. Hata CCM wanotafautiana na kutibuana sana, lakini si hadharani kama wafanyavyo Chadema, wao hufanya hivyo kwenye vikao halali vya ndani!

Ni aghalabu kusikia kiongozi wa CCM hususani wale wa ngazi ya juu akiropoka hadharani kwamba, Mwenyekiti, Makamu au Katibu Mkuu wake anafanya hili ama lile kwa masilahi ya



Kikao cha Kanda ya Nyasa kikiongozwa na Joseph Mbilinyi.

fulani au nia fulani ovu mbele ya kadamnasi ya watu!

CCM hutibuana, kuonyana na kuyamaliza huko kwenye vikao vya ndani, na wakitoka nje wote huongea lugha moja. Ukiona Mwana CCM kapewa 'kadi nyekundu' hadharani basi ujue huyo ameshindikana, yaani ni nunda!

Kwa mtaji huo basi ninawataka hapa Chadema wawaombe radhi Watanzania kwa kuwadanganya ikiwa ni kwa kutamka wazi kabisa kwa ndimi zao ama misikitini, makanisani au kwenye mikutano yao iwe ya ndani au ya hadhara kwamba CCM si kwenye udanganyifu nyakati za chaguzi bali kwao wao.

### TUMWACHE RAIS ACHAPE KAZI

Niongeze pia hapa kwamba wapinzani waliopitwa na wakati na walio na umahututi wa kisiasa kama Tundu Lissu, Freeman Mbowe kwa kuwataja wachache wanatakiwa kuacha figisu, badala yake kumpa uga mkubwa Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan aongoze nchi hii kwa amani na utulivu.

Nasema hivi kwa sababu, Rais wetu amekuwa na jitihada za kuturejesha kule ambako vijana wetu walikuwa wakisoma bure tangu chipukizi hadi chuo kikuu, wakitibiwa bure maradhi yoyote yale, na kikubwa kabisa ni kurejesha kulitumikia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa ajili ya kulinda adabu za vijana wetu, kuwa wazalendo na kuwa wamiliki wa afya njema na ustawi mwema.

Nani anabisha hapa nikisema kwamba kujuana zaidi kwetu kulitokana na kuweko JKT huku baadhi yetu tukijikuta hatuna uwezo wa kujizuia kujuana milele na kuwa ndugu au wazazi!

Kwa mtaji huu basi, hawa wapinzani uchwara waache unafiki wao wa kisiasa na kumwacha Dk. Samia ajikite kwenye uongozi wa haki na wa kweli.

Ni kweli, Rais Samia ni binadamu, anaweza kuwa na mapungufu lakini staha lazima iwapo kama una hoja ya kumfikishia.

Wanaompinga, tena bila staha wajue kuwa wako nyuma ya gharika kubwa kama zilivyowakuta wale wote waliowapinga wateule wa Mungu wetu.

Ni aibu kiasi gani kwa chama kikuu cha upinzani kuwa na viongozi wapiga mazingaombwe, halafu watu wa aina hii eti wanataka kuwa marais wa nchi hii tukufu ya Tanzania ambayo imekomboa nusu ya dunia nzima kupitia vikao vya kimataifa (UN) mpaka kwenye ardhi ya waliokuwa wakitawaliwa kwa mabavu na dhambi kama Msumbiji, Afrika Kusini, Angola, Namibia na Zimbabwe.

Poleni sana kina Lissu, Mchungaji Msigwa na wenzenu kama ninyi mnaokumbana na dhahama ya Mwenyekiti wenu Mbowe ambaye msamiati wa kung'atuka madarakani ili kupisha wengine yeye na genge lake hana.

### KUJITAFUTIA LAANA

Hata hivyo, nikiwa naelekea kutamatisha makala haya napebdq kuwaambia kwamba jamaa yenu Lissu anapitia na kukiona cha mtemakuni kwa kukosa radhi za Baba wa Taifa hili, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kitendo chake cha kumdhihaki kwenye Bunge la Katiba la mwaka 2014.

Mafundisho ya dini zetu yenye pumzi ya Mungu yanatutaka tusiwadharau wazazi wetu na waliotuzidi umri kwani tunaweza kujipa laana.

Kwa taifa hili, Nyerere ni baba na ndio maana anaitwa Baba wa Taifa. Mtu kapigania uhuru wa taifa lako halafu wewe Lissu kakusomesha bure kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu hata kama mwaka wako wa mwisho ulisoma kwa kupewa mkopo jumlisha matibabu ya bure kwa sababu enzi za Mwalimu matibabu yalikuwa bure halafu unakuja kumdhihaki! Laana haikuachi na namna ya kuondokana nayo ni rahisi tu. Kutibu na kuomba radhi.

Nimalizie kwa kumwombea mema Rais wangu. Mungu atakulinda Dk. Samia dhidi ya binadamu hawa wenye vijiba vya roho na visolokwino. Tunaona jinsi unavyoifanya Tanzania leo hii ili kurejea kwenye utukufu wake. Unafanya yote haya si kwa uchawi wala shiriki bali kwa ridhaa na karama za mwenyewe Jalali ambaye unamwomba usiku na mchana akujaalie wewe, familia yako na Watanzania wote wakiwemo wapinzani wanaokubeza!

Mungu akulinde na ubaya wote iwe hapa duniani na/au kesho akhera.

Kwani kwa uadilifu wako na nia yako safi Mwenyezi Mungu Mtukufu atakulinda na kila shari.

Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.



Tundu Lissu



# Tunapozungumzia uharibifu wa misitu tusisahau kilimo

**Na Hamisi Kibari**

JUNI 5 wiki iliyopita ilikuwa Siku ya Mazingira Duniani ambapo iliadhimishwa kitaifa pale Dodoma huku maeneo mengine nchini pia yakiiadhimisha kwa namna tofautitofauti.

Kuna walioiadhimisha kwa mihadhara ya kukumbushana umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira, kuna walioiadhimisha kwa kufanya usafi katika maeneo yao, kuna walioiadhimisha kwa kupanda miti na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo utaona mazingira ni dhana pana ikuhusisha uchafu na wachafu, umuhimu wa kuzungukwa na uoto na ndio maana tunapanda miti, na hata masuala ya kelele ni suala pia linalohusu mazingira yetu.

Katika makala haya ninakusudia kuzungumzia suala la umuhimu wa kuhifadhi misitu ambalo kwa mtazamo wangu lilijitokeza sana. Misitu ni nini? Ni mkusanyiko wa uoto unaojumuisha miti mingi ambamo pia hupatikana mimea mbalimbali zikiwemo nyasi fupi au ndefu. Ndani ya misitu pia kuna viumbe hai kadha wa kadha.

Misitu inaweza kuwa ya asili ikiwa na miti mbalimbali kama vile mipingo, mikoko, miyombo, migunga na mingine mingi au yaweza kuwa imetokana na miti ya kupandwa na binadamu kama misaji, mikaratusi na kadhalika. Misitu ya asili ni kama vile msitu wa Udzungwa ulioko Morogoro na ya kupadwa ni kama vile Tongwe na Nilo iliyoko Muheza na Korogowe mtawalia, mkoani Tanga.

## FAIDA ZA MISITU

Misitu ina faida nyingi kwa mwanadamu na viumbe wengine, baadhi ya hizo ni kunyonya hewa chafu na kutoa hewa nzuri kwa mwanadamu, kusababisha vyanzo vingi vya maji, kuwa makazi ya viumbe mbalimbali na ndani ya misitu hupatikana aina mbalimbali za miti ikiwemo miti dawa au inayotoa mbao.

Misitu pia hutupatia nishati ya kupikia (kuni na mkaa) husaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo, huwezesha ufugaji wa nyuki huwa chanzo cha kuvuta mvua na pia misitu ni kivutio cha utalii. Kwa mantiki hiyo, mwanadamu hutegemea sana uwepo wa misitu kwa mustakabali wa maisha yake kutokana na faida lukuki anazopata. Kwa lugha nyingine misitu ni uhai.

## MADHARA YA KUMALIZA MISITU

Pamoja na umuhimu huo wa rasilimali misitu, dunia imeendelea kushuhudia uharibifu mkubwa wa misitu ambao unatokea kila kukicha, hali ambayo inatoa ujumbe wa hatari kwa siku zijazo kuhusu mazingira.

Mbali na kukosa faida luluki za misitu pale inapoharibiwa kama ilivyoelezwa tayari, kuna tatizo kubwa ambalo dunia inakabiliana nalo sasa la mabadiliko ya tabianchi, linalochangiwa kwa kiwango kikubwa na uharibifu wa mazingira ikiwemo uharibifu wa misitu, hali ambayo inasababisha ongezeko la joto duniani.

Nchini Tanzania, kwa takwimu zilizopo kiasi cha hekta 469,420 za misitu, ukubwa ambao ni maradufu ya ukubwa wa jiji la Dar es Salaam, hupotea kila mwaka nchini Tanzania kutokana ukataji wa miti usio endelevu.

## NINI KINACHOMALIZA MISITU?

Watu wengi ukiwauliza swali ni kitu gani hasa kinachoongoza kwa kusababisha uharibifu mkubwa wa misitu, watatupa lawama kwenye ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa, mbao au kuni. Hata kwenye mijadala mingi ya Wiki ya Mazingira hadi siku ya kilele, Juni 5, mijadala mingi ilijielekeza kwenye watu kuaminishwa kwamba ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa ndivyo vinaongoza kwa kumaliza misitu nchini.

Lakini ukweli si hivyo. Unashangaa? Sikia maelezo. Kinachoongoza katika kumaliza misitu kwa mujibu wa tafiti zilizopo ni kilimo, hususani kilimo cha kuhamahama. Kwamba wakati ukataji mkaa unaweza kuruhusu msitu kuota upya, kilimo huondoa kabisa msitu!

Kwa lugha nyingine, pori linaweza kukatwa miti yote kwa ajili ya mbao, kuni na mkaa lakini kama halitaguswa tena kwa miaka kuanzia 12 na kuendelea, litarudi tena kuwa msitu. Lakini ukishageuza eneo hilo kuwa shamba, sahau kurudi kuwa msitu!

Pamoja na watu kutegemea raslimali za misitu kuendesha maisha yao, asilimia kubwa ya Watanzania hutegemea kilimo ili kujipatia mahitaji yao ya kila siku. Kilimo hutoa chakula, kilimo ni biashara na kilimo hutoa mali ghafi kwa ajili ya viwanda vyetu.

Kilimo katika nchi za Afrika ambazo ziko nyuma katika utumiaji wa teknolojia za kisasa unaowezesha eneo dogo kuzalisha mazao mengi, kimekuwa kila wakati ni chenye kuhitaji eneo kubwa. Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Charles Meshack anasema mahitaji ya ardhi kwa ajili ya mashamba ya kilimo yanachangia upotevu wa misitu kwa asilimia 80 wakati mkaa ambao unanyooshewa sana kidole ni chini ya asilimia 10.

Meshack alibainisha hayo wakati fulani alipozungumza na wabunge wa Jamhuri ya Muungano ambao ni wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii jijini Dodoma. Bahati nzuri mimi (mwandishi wa makala haya) nilikuwepo. Alisema siku hiyo kwamba kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanywa na TFCG na taasisi nyingine zimeonesha upotevu mkubwa wa misitu nchini unasababishwa na kilimo hasa cha zao la mahindi.

Akasema asilimia kubwa ya upotevu huo unatokea hasa katika maeneo ambayo misitu yake haina mfumo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (USMJ).

Meshack anasema utafiti unaonesha kuwa Tanzania ina jumla ya hekta milioni 48 za misitu ambapo asilimia 47 ya misitu hiyo ipo katika ardhi za vijiji na kwamba ni hekta milioni mbili pekee ndizo zipo kwenye usimamizi shirikishi (USMJ). Meshack anasema iwapo hakutakuwa na jitihada za kuilinda, kuitunza na kuindeleza, baada ya miaka 40 ijayo misitu itatoweka kabisa nchini.

Mkurugenzi huyo anasema mfumo wa USMJ umeweza kuchochea uhifadhi, ulinzi na utunzaji huku maendeleo yakipatikana. "Ushahidi upo kuwa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii umeweza kuongeza thamani mazao ya misitu nchini, lakini pia miradi ya elimu, afya, maji, uhifadhi ikifanikishwa kwa uendelevu," anasema.

## USIMAMIZI SHIRIKISHI UNAFANYIKAJE?

Usimamizi shirikishi ni pale wananchi, wanapowezeshwa kupitia elimu kuona manufaa ya msitu unaowazunguka na kugeuka kuwa walinzi thabiti wa msitu huku wakivuna raslimali za misitu kwa njia endelevu. Mfano wake, wakati akizungumza ulikuwa unapatikana katika vijiji zaidi ya 30 katika wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro vijijini mkoani Morogoro ambako vijiji vingine nchini vinaweza kwenda kujifunza.

Vijiji hivyo, kwanza vina mpango wa matumizi bora ya ardhi. Baada ya kupimwa kijiji hutenga eneo kwa ajili ya msitu, eneo la mashamba, malisho, makazi na huduma za jamii. Kupitia mradi wa Kuleta Mabadiliko Katika Sekta ya mkaa nchini (TTCS), vijiji hivyo viliwezeshwa na TFCG kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kuzalisha mkaa kwa njia endelevu.

Baada ya kumalizika kwa mradi wa TTCS katika vijiji hivyo darasa, sasa TFCG na Mjumita wakawa wanaendesha mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu (CoForEST). Kinachofanyika msituni ni eneo la asilimia 10 la msitu wa kijiji ndilo hutengwa kwa ajili ya uzalishaji mkaa miaka yote. Mkaa huzalishwa kitalaamu kwa kuruhusu miti kukua na kuzaliana upya na hivyo uzalishaji kuwa endelevu. Pia uchomaji wa mkaa hutumia tanuri kichuguu ambalo hutoa mkaa mwingi mzuri.

*Inaendelea uk.18*

# Uhuru usiokuwa na mipaka ni wendawazimu

**Na Hamid Yassin**

KWANZA kabisa nimpongeze na kumtakia maisha marefu Rais Samia Suluhu Hassani kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake Machi 19 mwaka huu.

Kwa mtaji huo basi nimtake Rais Dk. Samia ajisikie salama kabisa na kumtaka akabiliane na changamoto nyingi za kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati na viwanda kama ilivyokuwa wakati.

Kwa nini nimesema changamoto? Ndiyo; changamoto kwa sababu wamezuka watu wanaojiita wanaharakati wa haki za binadamu wanaomshutumu Rais wetu kwa mambo mbalimbali yasiokuwa na kichwa wala miguu.

Kwa kweli binafsi nilipowasikia watu hao wakiongopa kwamba kwenye Awamu hii hakuna uhuru wa vyombo vya habari, nilirudi nyuma zaidi wakati wa Utawala wa Awamu ya Pili wa hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi.

Kwa waliokuwepo wakati huo watakumbuka kuwa utawala huo ulifuta magazeti matano hapa nchini baada ya kwenda kinyume cha wajibu wao.

Kwa nini nasema "wajibu wao?" Ndiyo, nasema hivyo kwa sababu katika dunia hii mtu akitaka haki lazima atimize wajibu. Kwa msemo mwingine ni kwamba "Hakuna haki bila wajibu".

Kana kwamba hiyo haitoshi, "hakuna uhuru usiokuwa na mipaka". Uhuru ni lazima uwe na mipaka kinyume chake huwa ni wendawazimu.

Basi, Kufutwa huko kwa magazeti hayo matano wakati wa Utawala wa Alhaji Mwinyi kulikuja baada ya baadhi ya waliokuwa wamejidai ni waandishi wa habari kumbe walikuwa wavamizi wa fani hiyo.

Nawaita wavamizi kwa sababu walikwenda mbali zaidi kiasi cha kumtukana kama siyo kumsingizia Mzee Mwinyi kuwa alikuwa amedharau kuongea na madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Ndipo kulipoanza sekeseke kubwa la matusi dhidi yake bila kukumbuka kwamba Mzee Ruksa ndiye aliyeruhusu vyombo vya habari binafsi kutamalaki hapa nchini, hivyo haikushangaza pale Serikali ilipoamua kuyafuta magazeti hayo na siyo kuyafungia.

Ilipokuja zamu ya Awamu ya Tatu ya hayati Benjamin William Mkapa baadhi ya waandishi hawakuacha kujikita katika maandishi ya fedheha na matusi dhidi yake.

Lakini kwa vile Mkapa alikuwa ni Mwandishi wa Habari kitaaluma tena makini hapa Tanzania na nje ya nchi, alichukua hatua mbalimbali za kufungia magazeti ya waandishi wa aina hiyo na ndipo aliposema kwa sauti kubwa dhidi ya hao waliojiita wanaharakati wa haki za binadamu.

Alisema, naomba nimnukuu; "Ukidai haki timiza wajibu". Akaongeza, "Hakuna uhuru usiokuwa na mipaka; hata hao Wazungu wanalijua hilo."

Basi, na mimi huo ndio msimamo wangu mkubwa wa makala haya kwa siku ya leo.

Ningewaomba waandishi wa habari tubadilike hasa kwenye kipindi kama hiki ambapo dunia inakwenda kombo sana baada ya kuvurugwa na mitandao ya kijamii. Mitandao ya kijamii? Ndiyo, hii sasa ndiyo inatuharibia mustakabali wa taaluma hii na nchi yetu kwa ujumla.

Tushukuru Mungu vyombo vya habari vingi hivi sasa vimetulia, ni mara chache sana kuona vimeibuka na habari zisizo na kichwa wala miguu, hasa kutokana na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dk. Samia kuwatendea sana haki ikiwemo kuvifungulia vile vilivyokuwa vimefungiwa kwa muda mrefu tangu awamu zilizotangulia na kuvitaka vijikite katika weledi hata vikikosoa serikali vifanye hivyo kwa staha.

Lakini huku kwenye mitandao ya kijamii ndiyo kumeibuka kama janga la taifa, kwa sababu huku si waandishi wa habari pekee wanaohusika kuweka maudhui mbalimbali, bali kila anayejua kusoma na kuandika ana mwanya wa kuandika chochote anachojisikia!

Wanasiasa, wanaharakati na wananchi wa kawaida wenye mahaba na vyama mbalimbali wanatumia fursa ya kuwepo kwa mitandao hii kuivuruga nchi yetu kwa kuweka maudhui ya ovyo kwenye mitandao hiyo kuliko yale ya kujenga.

Kwa hiyo ndipo ninaporudi palepale kwamba wanaharakati wa nchi hii na hata hao mabeberu hawana tija kabisa wanapodai kuwa uhuru wa vyombo vya habari hapa nchini umebanwa.

Zipo nchi kadhaa hasa zile za Asia na Mashariki ya mbali ambapo matumizi ya mitandao kwa raia wao yana mipaka yake huku nchi nyingine zikipiga marufuku kabisa.

Huku kwetu baadhi ya wananchi watumia vibaya hii fursa ya uhuru wa kutumia mitandao kufanya masuala ya ovyo kama vile kujiingiza kwenye uanaharakati uchwara na wa kipuuzi kwa kutumiwa na mabeberu kama walivyotumiwa kuwatukana Marais Mwinyi, Mkapa na sasa wanataka kumkosea adabu Rais wetu, Dk. Samia kwenye mitandao hiyo.

Mpaka hapa namwambia Rais Dk. Samia kuwa asitishwe na hao wanaojiita wanaharakati, si wa hapa ndani bali hata hao wa nje, wanaodai kwamba uhuru wa habari unabanwa hapa nchini.

Ni vyema wajue kuwa duniani kote taaluma ya habari kama zilivyo taaluma nyingine ina miiko yake. Bila kuitekeleza, hiyo si taaluma bali ni umaamuma!

Nawaambia hivi kuwa wewe Rais wetu si maamuma; unajua mambo mengi sana kuliko ukomo wa akili zao. Ndio maana unazo radhi za Mola na kinga yake dhidi ya maibilisi hao wanaojiita wanaharakati.

Si unafiki kusema kwamba Watanzania ni hodari kwa uongo na uzushi si tu barani Afrika bali wanaweza kuongoza duniani.

Katika miaka ya themanini na tisini jiji la Lagos nchini Nigeria lilisifika kwa uzushi na uongo kwa kisingizio cha wahitimu wa vyuo vikuu nchini humo kukosa ajira serikalini au kwenye mashirika na makampuni binafsi.

Wasomi hao waliokosa ajira serikalini walijiingiza kwenye shughuli za utapeli walifanikiwa kuutekeleza kwa weledi mkubwa kutokana na elimu yao.

Hali hii sasa imeanza kujikita kwa kasi ya ajabu nchini mwetu tangu Serikali iliporuhusu mitandao ya kijamii.

Mitandao hii imedhihirisha kile kinachoitwa uzushi na uongo uliovuka mipaka kutokana na kila mara kuzusha mambo ambayo kama hayatadhibitiwa yanaweza kuiingiza nchi kwenye taharuki au hata machafuko kabisa.

Tukumbuke kwamba Rwanda iliingia kwenye ghasia zilizopelekea kutokea mauaji ya kimbari mwaka 1994 kutokana na baadhi ya vyombo vya habari kusambaza uzushi uliotopea na kusababisha mauaji hayo.

Hii mitandao ya kijamii ya Tanzania haikuanza leo kuzua uongo, nakumbuka wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano ilianza kusambaza uzushi hatari pale ilipodai kuwa aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bi. Samia Suluhu Hassan alikuwa haelewani na aliyekuwa Rais hayati John Pombe Joseph Magufuli.

Mitandao hiyo, ambayo maudhui yake yalinukuliwa na baadhi ya magazeti, vituo vya redio na televisheni za hapa nchini, ilidai kuwa Makamu huyo wa Rais ambaye hivi sasa ndiye Rais wetu, alikuwa ameandika barua ya kujiuzulu wadhifa wake huo wakati si kweli!

Ukiacha uzushi, ikiwemo Dk. Philip Mpango wakati fulani kuzushiwa kifo, pia mitandao iliwahi kuzusha habari za upuuzi kwamba, hayati Magufuli alimtosa mtangulizi wake, Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Khalfan Kikwete.

Kwa muktadha huo basi, niseme hapa kuwa Serikali inaweza kulazimika kuifungia baadhi ya mitandao hiyo ya kijamii inayoandika uongo na uzushi ambayo inaweza kusababisha machafuko.

Hakuna ubishi kwamba baadhi ya mitandao hii imeamua kuwa mbadala wa vyama vya upinzani kuendesha siasa za ovyo na chuki dhidi ya CCM na Serikali yake.

*Inaendelea uk.18*

**Ukidai haki timiza wajibu. Hakuna uhuru usiokuwa na mipaka; hata hao Wazungu wanalijua hilo.**





# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Rais Samia anavyoweka alama isiyofutika nishati safi ya kupikia




Mahitaji ya msingi ya binadamu ni chakula, malazi na mavazi. Binadamu akiyapata mahitaji haya, anakuwa amekidhi mahitaji muhimu na hivyo kuendelea na mchakato wa kutafuta mahitaji mengine ya ziada kwa ustawi wa maisha yake.

Hitaji la chakula kwa mfano linakamilika pale ambapo chakula kinakuwa kimeandaliwa na kupikwa vyema tayari kwa kuliwa. Ili chakula kiive ni lazima kipikwe kwenye nishati ya kupikia kama vile kuni, mkaa, jiko la gesi au umeme na aina nyingine ya nishati kama mafuta ya taa, jua na kadhalika.

Hivyo, kukamilika kwa chakula kunategemea matumizi ya nishati ya kupikia katika maandalizi yake. Kutokana na hatua za kimaendeleo hasa nyanja za sayansi na teknolojia, utunzaji wa mazingira na kulinda afya za binadamu, upo umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupikia kama vile majiko yanayotumia gesi na umeme na kuachana kabisa na nishati chafu kama ya kuni na mkaa.

Kwa miaka mingi hasa katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, nishati chafu ya kuni na mkaa imekuwa ndiyo inatumika kwa asilimia kubwa kupikia mijini na vijijini. Matumizi makubwa ya kuni na mkaa yamekuwa na athari hasi katika jamii kutokana na kuharibu mazingira, kuhatarisha afya za binadamu na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Katika mambo ambayo naona Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ataacha alama isiyofutika Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla na kufanya jina lake kuandikwa kwa wino wa dhahabu wakati huu akiwa madarakani na hata baada ya kustaafu ni pamoja na hili la harakati anazozifanya kupambania kufanikisha mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Tanzania na Bara la Afrika.

Zipo harakati nyingi ambazo Rais Samia anafanya ambazo bila shaka zitaacha alama kubwa kama vile kuwarejesha shule wanafunzi waliopata changamoto mbalimbali shuleni ikiwemo mimba, kuhamasisha vijana wakiwemo wasomi kushiriki kwenye kilimo cha kisasa kupitia Jenga Kesho iliyo Bora (BBT), maboresho ya mitaala ya elimu inayojielekeza kwenye kuwawezesha watoto kumaliza shule wakiwa tayari wana ujuzi fulani na mengine lukuki.

Lakini leo imenipendeza kuangazia hili la nishati safi ya kupikia. Harakati anazozifanya Rais Samia katika eneo hili pekee zinaacha alama kubwa katika uongozi wake na hii ndiyo sifa ya kiongozi bora – kuacha alama.

Jambo hili la kiongozi kuacha alama amelisema pia Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa jijini Dar es Salaam katika mahafali ya saba wakati akiwatunuku astashahada na vyeti wahitimu 198 katika Taasisi ya Uongozi ambapo amewashauri waliohitimu uongozi kuwa na mipango na mawazo yatakayowezesha kuacha alama katika uongozi wao pale watakapomaliza muda au kuhamishwa.

"Watu watakukumbuka kwa lipi katika uongozi wako. Tujitahidi kuacha alama. Viongozi lazima wawe tayari kila wakati kutafuta suluhu za changamoto zinazoendelea kama vile umaskini, mabadiliko ya tabianchi, ujinga, shida ya chakula, magonjwa na mambo mengine wajikite kutatua kero zinazojitokeza," alisema Kikwete.

Ni ukweli kuwa Rais Samia ameona changamoto zinazosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa, ndiyo maana akachukua hatua za kuwa kinara wa kusukuma ajenda ya nishati safi ya kupikia.

Kwa mfano, kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, zaidi ya watu 32,000 hufariki dunia kila mwaka nchini kutokana na matumizi ya nishati chafu huku kila mwaka nchi ikipoteza zaidi ya hekta 469,420 za misitu kutokana na uharibifu unaochangiwa na ukataji miti kwa ajili ya kupata nishati chafu ya kupikia.

Ikumbukwe kuwa matarajio ya serikali ni kuwa hadi kufikia mwaka 2034, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Miaka 10 ijayo kuanzia sasa si mbali, ndiyo maana Rais Samia amekuwa akipaza sauti ndani na nje ya Tanzania kupigania matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Akiwa kwenye Mkutano Mkuu wa Nishati Safi ya Kupikia uliowakutanisha Marais, Viongozi na Wadau mbalimbali wa Afrika katika Makao Makuu ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) jijini Paris, Ufaransa, Rais Dk. Samia alisema zaidi ya Waafrika milioni 900 wanatumia nishati isiyo safi ya kupikia, jambo linalochangia uharibifu wa mazingira, upotevu wa bioanuai na athari za kiafya.

Katika Mkutano huo, Rais Samia alisisitiza kuwa kuongezeka kwa upatikanaji wa nishati safi ya kupikia itasaidia wanawake kupata fursa zaidi kushiriki shughuli nyingine za kiuchumi, kupunguza umaskini na usawa wa kijinsia.

### UTASHI WA KISIASA

Hakuna shaka kuwa Rais Samia amedhamiria kuiona Tanzania na Afrika ikiachana na nishati chafu na kutumia nishati safi na ndio maana kila anapopata jukwaa la kuongea na wananchi, ndani na nje ya nchi amekuwa akisisitiza ajenda ya nishati safi ya kupikia.

Kwa mfano, Mei 8, 2024, Tanzania ilizindua Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia ambapo mkakati huo umekusudia kufikia asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati safi ifikapo mwaka 2034 yaani miaka 10 ijayo kuanzia sasa.

Katika Mkutano huo nchini Ufaransa, Rais Samia alisema; "Serikali imelipa umuhimu suala la nishati safi ya kupikia ambapo katika kuyafikia malengo hayo bajeti kuu ya serikali imeweka kipaumbele katika kuwezesha upatikanaji wa nishati hiyo sambamba na kuwainua wanawake."

Wiki iliyopita, akiwa katika ziara ya siku sita nchini Korea Kusini Samia pia aliingiza ajenda ya nishati safi ya kupikia akiitaka nchi hiyo ambayo imepiga hatua kimaendeleo kuona namna itakavyoweza kusaidia katika suala zima la nishati safi ya kupikia."Kwa kuwa nimekuwa Rais Mtendaji pekee katika ukumbi huu sasa hivi, lazima nizungumze kuhusu ajenda muhimu ya Afrika na suala la mwanamke wa Afrika... Hili ni suala la kuwekeza katika nishati safi na salama ya kupikia," alisema.

Alisema Tanzania inapenda kusisitiza hitaji la kuimarisha ubia katika ushirikiano huu ili kuendeleza nishati safi ya kupikia. Alisema uwekezaji katika nishati safi ya kupikia siyo tu utapunguza utoaji wa hewa chafu na kulinda misitu bali pia unapunguza vifo vinavyotokana na matatizo ya upumuaji na kuwawezesha wanawake ambao ndio wapishi kufanya kazi zao kwa usalama zaidi. "Ajenda ya uwekezaji katika nishati safi ya kupikia Afrika pia unatoa fursa za kukua kiuchumi katika maana ya kutafuta ufumbuzi wa upatikanaji wa niashati safi ya kupikia Afrika," alisema.

*Inaendelea uk. 18*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

# Dondoo muhimu juu ya dhana ya kufanikiwa

**KUWA NA WAZO NA HAKIKISHA LIMEANDIKWA (HAVE AN IDEA WRITE IT DOWN)**

Baada ya kuwa na wazo na kuliandika, hatua inayofuata kulihusu wazo lako ni kuanza utafiti juu ya wazo lako ili kujua kama ni wazo la maana au hatakiwi kuendelea nalo (viability). Kama wewe unasoma dondoo hii, jiulize, una wazo gani kuhusu maendeleo yako? Usiridhike kuishi bila wazo lako mwenyewe na kama huna, anza sasa kujitafuta na shirikisha hata washauri wakusaidie. Hakuna mafanikio bila kuwa na wazo la mafanikio.

**TENGA MUDA AMBAO UTAFANYIA KAZI WAZO LAKO (HAVE A CLEAR TIMELINE OF GOALS)**

Usipoweka muda hutaweza kujipima. Jiwekee mipaka ya muda.

**JIFUNZE KWA WALIOTANGULIA KISHA UFANYE KWA UBORA (INVEST TIME IN LITERATURE REVIEWS)**

Kama kuna habari zinazohusiana na wazo lako nenda usome. Kama kuna waliokwisha fanya, wasikilize. Usikimbilie tu kuanza, kama kuna jinsi ya kupata taarifa basi zitumie kwanza. Taarifa mbalimbali zitakupa maarifa mengi ambayo hukuwa nayo unapowaza jambo, maarifa haya yatakupa kufanya kwa ubora.

**LIPANGE WAZO LAKO KWA KULIGAWA KWENYE MALENGO MADOGOMADOGO YENYE SIFA KUBWA TANO ZENYE UFUPISHO SMART (BREAK YOUR THESIS DOWN INTO "SMART").** Pata ufafanuzi wa maelezo haya.

**S SPECIFIC** - Uwe na Malengo Maalumu. Lenga kitu maalumu, usiweze mambo mengi bila kujua tija, lenga jambo mojamoja.

**M MEASURABLE** - Weka wazo kwenye malengo yanayopimika

**A ATTAINABLE** - Hakikisha wazo lako linatekelezeka.

**R RELEVANT** - Hakikisha ni wazo la maana na sahihi kwa wakati huu.

**T TIMELY** - Tenga muda maalumu kwa wazo kutekelezwa.

Hakikisha unatengeneza au kujiunga na mtandao wa watu wenye maono kama yako (Get the network of the people with your vision)

Ni rahisi kupata mafanikio ukiwa na watu wenye malengo na maono kama wewe. Mafanikio yako yanategemea sana na watu waliokuzunguka. Hili ni suala ambalo matokeo yake huwa hayaonekani mapema lakini kama ukikosea kwenye eneo la marafiki au mtandao wako, unafeli haraka.

**ANZA SASA KULITEKELEZA WAZO LAKO (START NOW)**

Kuwa na wazo na kutekeleza wazo ni vitu viwili tofauti. Wengi wana mawazo lakini wanaotekeleza ni wachache. Ukipata wazo na kupitia hatua zote hapo juu kwa mtiririko wake, usingoje kesho wala usiahirishe, anza sasa, kwa maana nyingine, anza haraka.

**KUWA MBUNIFU, ACHA WOGA, USIISHI KWA MAZOEA, FIKIRIA NJE YA UKAWAIDA (THINK OUTSIDE THE BOX DO NOT BE AFRAID)**

Mafanikio yanahitaji mambo haya. Na mambo haya yanafanyika baada ya kuanza. Ulianza kutekeleza wazo lako ukakosa sifa hizi, utaishia kuwa wa kawaida. Ubunifu ndiyo humtofautisha na wengine

**PATA WATU SAHIHI UTAKAOSHIRIKIANA NAO AMBAO WATAKUSAIDIA KULIFIKIA LENGO (GET PEOPLE WHO CAN HELP TAKE YOU THERE) KWA KUZINGATIA MASLAHI YA PANDE ZOTE (IN A WIN WIN SITUATION)**

Hata kama wazo ni dogo, utahitaji watu kukusaidia. Ni muhimu kuwa makini kuhakikisha vitu vyote muhimu vimezingatiwa wakati wa kufanya maamuzi hayo sababu aina ya watu utakaokuwa nao ndiyo aina ya mafanikio ya wazo lako.

Hamasa ya somo hili ni kukupa azma ya kuandaa mafanikio yako mwenyewe.

Kama unataka kufanikiwa, lazima uwe na wazo la kukufikisha kwenye mafanikio unayoyahitaji. Bila kuwa na wazo lolote ila unawaza kupata kazi na mshahara pekee, sahau kabisa neno au dhana ya mafanikio ya ziada maishani mwako.

Sikwambii kuwa itakuwa rahisi, ila lazima uwe na wazo na ujipange kwa mujibu wa kanuni za mafanikio ndipo uingie kwenye safari ya wanaohitaji kufanikiwa.

Kama unapenda kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi Binafsi au ya Serikali, Kikundi cha kijamii, Kanisa, Umoja, NGO, Mtu binafsi n.k) Karibu tuwasiliane

Wework Consult - Your Partner in Growth.



# Rais Samia anavyoweka alama

*Inatoka uk.16*

Alisema Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina na yeye, wemekuwa wakiifanyia kazi ajenda hiyo ili kupata fedha na kwa msingi huo akaiomba Serikali ya Jamhuri ya Korea kujiunga nao katika suala hilo muhimu.

Dhamira ya Rais Samia ya kutaka ajenda ya nishati safi ya kupikia ifanikiwe Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla imewafanya wabunge, watu binafsi, kampuni binafsi na taasisi zisizo za serikali (NGOs) kutoa misaada wa majiko ya gesi bure kwa mama lishe na wajasiriamali wengine kama mkakati wa kuepukana na matumizi ya nishati chafu. Jambo hili limefanyika na linaendelea kufanyika nchi nzima katika kumuunga mkono Rais Samia na ajenda ya nishati safi ya kupikia.

**BWAWA LA NYERERE NA NISHATI SAFI YA KUPIKIA**

Serikali inatarajia kutumia Shilingi trilini 6.6 hadi kukamilisha mradi wa Bwana la Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) ambapo mradi huo unatarajiwa kuzalisha megawati 2115 za umeme ambazo zitasaidia sana kupunguza tatizo la umeme nchini na kuchangia maendeleo ya viwanda na uchumi kwa ujumla.

Nishati safi ya kupikia inahusisha pia matumizi ya majiko ya umeme, kwahiyo kukamilika kwa mradi huu wa umeme kutasaidia pia kuongeza wigo wa matumizi ya nishati safi ya umeme.

Ushauri wangu kwa serikali ni huu, Mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere utakapokamilika na kuzalisha megawati zote 2115, serikali ipunguze bei ya umeme ili kuwawezesha Watanzania wengi kutumia nishati safi ya majiko ya umeme katika kupikia huku wakichanganya na majiko ya gesi ili kutokomeza kabisa matumizi ya nishati chafu kama kuni na mkaa.

Kusema ukweli, asilimia kubwa ya Watanzania, hasa waishio mijini wana umeme lakini kwa nini hawatumii majiko ya umeme? Bila shaka sababu kubwa ni gharama kubwa ya umeme. Hata kwenye nyumba zetu nyingi hizi za kupanga si rahisi kukuta matumizi ya umeme kwa ajili ya kupikia yakiruhusiwa. Hata mwenye nyumba akikubali si rahisi wapangaji wenzako wakakubali!

Bei ya umeme na gesi vinapaswa kuwa chini kuliko kuni na mkaa ili wananchi waone umuhimu wa kutumia nishati safi ya bei nafuu na kuachana kabisa na nishati chafu katika kupikia. Kufanyike pia utaratibu wa gesi ambao utawezesha mtu kununua gesi hata akiwa na Sh 1000, kwa maana hiyo wahusika waangalie uwezekano wa hilo.

Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusambaza umeme mijini na vijijini, hali inayoifanya Tanzania kuwa kinara Afrika kwa usambazaji wa umeme kwa wananchi. Na ndiyo maana Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia (WB) nchini, Nathan Belete amesema Benki hiyo inatambua kazi nzuri zinazofanywana Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika masuala ya nishati.

"Hapa Afrika, Tanzania ni mfano mzuri katika usambazaji wa nishati ya umeme kwa wananchi. Tumejipanga kuwa na mazungumzo zaidi na kuona namna bora zaidi ya kusaidia katika masuala ya nishati safi ya kupikia kwa kufadhili na kuhusisha sekta binafsi kwa kuangalia fursa zilizopo," amesema Belete.

Ni jambo la faraja kuona juhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika kusambaza nishati ya umeme kwa wananchi zinatambulika kitaifa na kimataifa. Kwahiyo, umeme huo unaosambazwa kwa wananchi haupaswi kuwa ni kwa ajili ya kupata mwanga usiku, kuangalia runinga na kusomea tu, bali pia uwe ni chanzo cha nishati safi ya kupikia.

Na hii, kama nilivyokwisha sema, itafanikiwa endapo bei ya umeme itashuka kwa kiasi kikubwa hasa baada ya kukamilika mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere litakalozalisha megawati 2115 na pia kuibuliwa na kuendelezwa kwa vyanzo vingine vipya vya nishati ya umeme ukiwemo umeme wa jotoardhi unaotafitiwa kule Mbeya.

Rais wangu, Dk. Samia, nikutie moyo uendeleze mapambano haya ili kufikia mafanikio makubwa kabisa ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Ninawaomba Watanzania wenzangu wakiwemo wapinzani wako kisiasa wakuunge mkono angalau hata katika hili. Haiwezekani wao wawe wanakalia kulalamika tu na kutafuta tu makosa wakati mwingine kwa tochi bila kuunga mkono mambo mazuri kama haya na huo ndio uungwana.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

# Uharibifu wa misitu

*Inatoka uk.14*

Katika eneo hilo la asilimia 10, kunatengwa vitalu vya mita 50 kwa 50 vinavyovunwa kwa kuruka. Kama kitalu A kinavunwa leo, B kinarukwa hadi C na B kitarejewa baada ya miaka 12 katika mzunguko wa miaka 24 ambapo kitalu kilichokatwa leo huwa kimerejea kuwa msitu mkubwa. Miti yenye sifa tu ndio inayovunwa kwa ajili ya mkaa. Miti inayofaa kwa mbao inaachwa au iliyo katika vyanzo vya maji au makazi ya viumbe wengine kama nyuki pia haiguswi.

Hatua hii ilikuwa ya kipindi cha mpito kutokana na ukweli kwamba wakati nchi ikipambana kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia, pengine itatuchukua miaka kadhaa kuondokana kabisa na matumizi ya mkaa na kuni. Kwa mantiki hiyo ni vyema katika kipindi hiki kukawa na uvunaji endelevu wa kuni na mkaa badala ya uvunaji holela wa nishati hiyo ya enzi na enzi.

**JE, WANANCHI WAACHE KILIMO?**

Wanachi katika vijiji hivyo pia wamejifunza kilimo hifadhi kinachowawezesha kulima eneo dogo kisasa ili kupata mazao mengi. Wamejifunza pia ufugaji wa kisasa wa nyuki na kufungua vikundi hisa vya kuweka na kukopa. Hatua hizo zinasaidia kuwapa kipato mbadala badala ya kutegemea misitu kiwa kiwango kikuwa. Asilimia 60 ya mapato ya kijiji hutumika kulinda misitu kupitia kamati mbalimbali na asilimia 40 hupelekwa kwenye miradi ya maendeleo ambayo Meshack aliitaja kwamba ni pamoja na ujenzi wa shule, madarasa, kulipia bima wananchi na mingineyo.

Ukitembelea vijiji hivyo utagundua kwamba misitu inalindwa vyema kulinganisha na vijiji visivyo na USMJ na hii inaonesha kwamba wananchi wanaposhirikishwa na kuona faida ya kufanya uzalishaji endelevu, huwa ndio walinzi namba moja wa misitu yao. Kimsingi, tukitaka kunyanyua kilimo hatuwezi kuacha kufanya mabadiliko makubwa ya kilimo yatakayotuweza kulima kwenye eneo dogo kwa mavuno mengi.

Bahati nzuri serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeshaliona na ndio maana inawekeza kwenye kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, kuboresha shughuli za ugani, kuja na mbegu bora kupitia taasisi za utafiti kama TARI, na hata kuwa tayari kutoa ruzuku kwenye mbolea. Miradi kama ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ni muhimu sana katika kuwafundisha vijana wetu kuendesha kilimo cha kisasa ambapo wanaunganishwa na vyombo vya fedha kwa ajili ya mitaji itakayowawezesha kilimo cha kisasa.



Kufuatia safari ya Rais Samia Korea Kusini, ni habari njema kusikia kwamba kwa kushirikiana na wawekezaji... 

Kufuatia safari ya Rais Samia Korea Kusini, ni habari njema kusikia kwamba imewakaribisha wawekezaji kutoka nchini humo kuwekeza katika maeneo mawili; kilimo na madini. Akitoa ufafanuzi kuhusu ziara hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo amesema mbali na kusaidia katika utafiti, uwekezaji kutoka nje ikiwemo Korea utajikita katika kuzalisha bidhaa za kilimo na madini hapa hapa Tanzania na si kusafirisha nje mali ghafi.

Amesema umri wa Korea Kusini ni sawa na Tanzania na kwamba walianza maendeleo yao kwa kufanya mapinduzi katika kilimo, kisha wakafanya mapinduzi ya viwanda na sasa wako kwenye mapinduzi ya teknolojia. Kwetu sisi Watanzania tunapaswa kwenda navyo vyote, yaani kufanya mageuzi au mapinduzi ya kilimo, viwanda na kwenye teknolojia.

Kwa kifupi ninachosema hapa ni kwamba wakati tukidhibiti matumizi makubwa ya mkaa na kuni ambayo pia yamedhihirika kuwa na matatizo ya kiafya, tusidhani ni salama pia kufungua mashamba kila kukicha kwa gharama ya kufyeka misitu. Vyote tunavihitaji na hivyo suluhisho ni kuboresha kilimo ili tulime sehemu ndogo na kuvuna kingi. Ninajua hii dhana ngumu kidogo kuilewa lakini kama hujaelewa

# Uhuru usiokuwa na mipaka

*Inatoka uk.15*

Nasema hivi kwa sababu mengi ya maandishi ya mitandao hiyo ya kijamii yamekuwa sawa na mikutano ya wapinzani wasiokuwa na shukurani ya aina yoyote ile hata wakati serikali ikifanya mema kwa nchi na jamii yetu.

Kwa jinsi hiyo niiombe Serikali yetu makini isifanye ajizi kabisa kwa kuiacha mitandao hiyo kujipachika wadhifa wa upinzani dhidi yake.

Kwani mitandao hiyo inapoandika mambo ambayo ni hatari kwa usalama wa nchi yetu kama hayo niliyoandika na mengine ya uongo kama huo, kamwe haiwezi kuvumilika kwani huo ni uchochezi kama uchochezi mwingine wowote ule!

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema hivi, "Hakuna uhuru



usiokuwa na mipaka. Uhuru usiokuwa na mipaka ni sawa na wendawazimu au ukichaa".

Wakati Mwalimu Nyerere akiyasema hayo, Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa aliwahi kuwaambia waandishi wa habari waliokuwa wakiandika mambo bila mpangilio wala ukweli na kudai kubanwa kwa haki zao, "Haki haiji bila wajibu" kama nilivyoandika hapo awali.

Nami nishindilie msumari wa moto hayo kwa kuiomba Serikali isipuuze lugha mbaya za mitandao hiyo isiyotimiza wajibu wake wa kuielimisha jamii au kuipasha jamii ukweli wa mambo kwa kuzingatia zaidi utaifa, umoja na usalama wake.

Nasema hivi kwa sababu kinyume cha hivyo nchi hii itaingia kwenye machafuko makubwa yatakayowafanya wananchi wake kuwa wakimbizi ndani au nje ya nchi yao kama vile Wanyarwanda, Warundi, Wasudani Kusini, Wasomali, Watunisia, Wamisri, Wasyria, Wairaki, Walibya na kadhalika.

Matatizo yote hayo huanzishwa polepole na habari za kuzua na chuki na hasa wakati huu nchi hii inapoelekea kwenye chaguzi mbalimbali za ustawi wa taifa letu.

Mahasimu hao wa serikali na Taifa, kama kina Mange Kimambi wanatumia vibaya fursa ya mitandao kuwachochea wananchi kufanya vurugu za maandamano na mapigano yasiyokuwa na kichwa wala miguu. Waathirika wakubwa wa upuuzi huo huwa ni watoto, wazee na wanawake.

Nathubutu kusema hapa kwamba mitandao inayochochea vurugu na kuzua au kuwatukana viongozi wetu idhibitiwe kwa kunyimwa nguvu kubwa ya kufanya wanachotaka kwenye taifa hili.

***Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.***

# Makamu wa Rais wa Malawi athibitika kufa ajali ya ndege



**LILONGWE, Malawi**

MAKAMU wa Rais wa Malawi, Saulos Chilima na watu wengine tisa, wamefariki dunia baada ya mabaki ya ndege iliyombeba, kupatikana bila mtu yeyote aliyenusurika.

Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, alisema Chilima na wengine hao tisa, walikuwa wakisafiri nchini humo juzi asubuhi wakati ndege yao ilipotoweka kwenye rada za uwanja wa ndege.

Ndege hiyo kijeshi, ilikuwa ikisafiri hali mbaya ya hewa.

Wanajeshi walikuwa wakipekua Msitu wa Chikangawa katika juhudi za kuitafuta.

Katika kikao na wanahabari juzi Jumanne, Rais Chakwera alisema Kamanda wa Jeshi la Ulinzi la Malawi alimweleza kuwa shughuli ya utafutaji na uokoaji imekamilika na ndege hiyo kupatikana.

Chakwera alisema "alihuzunishwa na kusikitika sana" kuwafahamisha Wamalawi kuhusu mkasa huo mbaya.

Alisema timu ya uokoaji ilikuta ndege hiyo ikiwa imeharibika kabisa.

Makamu wa Rais na Rais, wanatoka vyama tofauti, lakini wawili hao waliungana kuunda muungano wakati wa uchaguzi wa mwaka 2020.

# Baraza la UN launga mkono usitishwaji vita Israel, Gaza



**NEW YORK, Marekani**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN), limepiga kura kuunga mkono mpango unaopendekezwa na Marekani wa kusitisha mapigano kati ya Israel na Gaza.

Pendekezo hilo limeweka masharti ya kusitisha mapigano kamili, kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa na Hamas, kurejeshwa kwa mabaki ya mateka waliokufa na kubadilishana wafungwa wa Kipalestina.

Wajumbe 14 kati ya 15 wa Baraza la Usalama, walipiga kura kuunga mkono azimio hilo lililoandaliwa na Marekani. Urusi ilijizuia.

Azimio hilo linasema kuwa Israel imekubali pendekezo la kusitisha mapigano na kuwataka Hamas kukubaliana nalo pia.

Ina maana Baraza la Usalama linaungana na serikali kadhaa pamoja na kundi la mataifa tajiri zaidi duniani la G7, katika kuunga mkono mpango wa sehemu tatu ambao ulizinduliwa na Rais wa Marekani, Joe Biden, Mei 31, mwaka huu.

Kura hiyo huenda ikaongeza shinikizo kwa pande zote mbili kujibu vyema mpango huo kwa nia ya kumaliza mzozo huo.

Pia hatua hiyo inajiri muda mfupi baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, kukutana na viongozi wa kigeni, akiwemo Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, katika jaribio la kujenga uungwaji mkono kwa mpango huo wa amani.

Saa chache kabla ya kura ya UN, Blinken alisema ujumbe wake kwa viongozi katika eneo hilo ulikuwa: "Ikiwa unataka kusitishwa kwa mapigano, washinikize Hamas waseme, ndiyo."

BBC.

# 38 wafa baada ya mashua kuzama

**ADEN, Yemen**

TAKRIBAN watu 38 kutoka eneo la upembe wa Afrika, wamefariki dunia baada ya mashua yao kuzama katika pwani ya Yemen, maafisa wa eneo hilo wamesema.

Walionusurika wamewaambia waokoaji kuwa mashua hiyo iliyokuwa imebeba takriban watu 250, ilizama kutokana na upepo mkali.

Msako unaendelea kuwatafuta karibu watu 100 ambao bado hawajapatikana.

Mamlaka za mitaa huko Rudum, Mashariki mwa Aden, zilisema kwamba waliokuwemo walikuwa wahamiaji, wengi wao kutoka Ethiopia, ambao hutumia Yemen kama njia ya kupita kuelekea maeneo ya Ghuba.

Hadi Al-Khurma, Mkurugenzi wa Wilaya ya Rudum, ameliambia Shirika la Habari la Reuters kuwa boti hiyo ilizama kabla ya kufika ufukweni.

"Wavuvi na wakazi, walifanikiwa kuwaokoa wahamiaji 78, ambao waliripoti kuwa wengine 100 waliokuwa nao kwenye boti moja, hawapo.

"Msako bado unaendelea na Umoja wa Mataifa umearifiwa kuhusu tukio hilo," alisema.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, wahamiaji 97,000 waliwasili Yemen kutoka upembe wa Afrika mwaka jana.

Ongezeko hilo limetokea licha ya vita nchini Yemen na mashambulizi ya hivi karibuni ya Wahouthi dhidi ya meli zinazopitia Bahari Nyekundu. BBC.



# Kundi la wenye silaha laua 25 na kujeruhi

**ABUJA, Nigeria**

TAKRIBAN watu 25 wameuawa na wengine kutekwa nyara na watu wenye silaha katika Jimbo la Katsina Kaskazini Magharibi mwa Nigeria, mamlaka zimesema.

Makumi ya watu waliokuwa na bunduki wakiwa na pikipiki, walivamia eneo la Yargoje huko Kankara Jumapili jioni, Kamishna wa Masuala ya Usalama wa Serikali, Nasiru Babangida Mu'azu, aliambia BBC Hausa.

Mashambulizi ya magenge yenye silaha yanayojulikana kama majambazi Kaskazini-Magharibi na katikati mwa Nigeria yamekuwa ya kawaida, na mamlaka inaonekana kukosa uwezo wa kuyazuia, licha ya madai ya serikali na vikosi vya usalama kwamba wanafanya kazi kumaliza ukosefu wa usalama ulioenea.

Wakazi waliambia BBC kwamba makumi ya watu waliokuwa na bunduki wakiwa kwenye pikipiki, waliingia katika jamii, wakifyatua risasi kiholela na kupora maduka kabla ya kuwateka nyara idadi isiyojulikana ya wanakijiji."

Watu waliouawa na majambazi ni zaidi ya 50, kwa sababu baadhi ya maiti bado zinatolewa porini, alisema mkazi mmoja ambaye hakutaka jina lake litajwe.

"Waliwaua watoto, wanawake na wanaume na kuteka nyara idadi kubwa ya watu. Waliwajeruhi zaidi ya wakazi 30 ambao kwa sasa wanapata matibabu katika hospitali kuu.




Mkazi mwingine, Abdullahi Yunusa Kankara, aliiambia Reuters kwamba aliponea chupuchupu mashambulizi hayo, ambayo alisema yaliendelea hadi saa za alfajiri ya Jumatatu.

"Mji wetu umegeuka kuwa eneo la kifo. Takriban kila nyumba kijijini, imekumbwa na shambulio hili. Maiti zaidi zilipatikana (Jumatatu) asubuhi," alisema.

Wakazi walionusurika wanajaribu kubaini ni watu wangapi wametekwa nyara.

Desemba, 2020, zaidi ya wanafunzi 300 walitekwa nyara kutoka shule ya sekondari ya wavulana ya bweni nje kidogo ya Kankara na genge la watu wenye silaha waliokuwa wakiendesha pikipiki.

Baadaye waliachiliwa, wiki moja baada ya serikali ya Jimbo la Katsina kuthibitisha kuwa walikuwa kwenye mazungumzo na watekaji nyara.

Machi, mwaka huu, makumi ya abiria walitekwa nyara katika shambulio la mchana pia katika eneo hilo hilo la Katsina, jimbo ambalo rais wa zamani wa Nigeria Muhammadu Buhari anatokea.

# Historia ya bendi ya Mlimani Park Orchestra-2

## ● Mtindo wake wa muziki ni 'Sikinde Ngoma ya Ukae'

**Na Mwandishi Maalumu**

### MWAKA 2007: UJERUMANI NA UHOLANZI

Walishiriki jumla ya matamasha mane (ambayo yote yanapatikana live kwenye YouTube) ambapo walipanda jukwaani Julai Mosi kwenye Tamasha la Afrika-Festival, Hertme kule Uholanzi, Julai 4 wakashiriki Tamasha la Masala-Festival jijini Hannover Ujerumani, Julai 7 wakapanda tena jukwaani kwenye Tamasha la Folk Festival mjini Rudolstadt Ujerumani kabla ya kumalizia ziara yao Julai 8 kwenye Tamasha la Folk Festival kule Rudolstadt Ujerumani.

### MWAKA 2012 MAREKANI

Mwezi Julai mwaka 2012, wanamuziki Hassan Rehani Bitchuka na Ally Jamwaka walipata safari ya kwenda nchini Marekani na kuzuru chuo kikuu cha Florida kwa udhamini wa Mmarekani Frank Gunderson (Associate Professor of Ethnomusicology, College of Music at Florida State University).

Wakiwa huko walipata nafasi ya kufanya mahojiano ambayo yalitumika kuandika kitabu kinachojulikana kwa jina la "The Legacy of Tanzanian Musicians Muhidin Gurumo and Hassan Bitchuka".

Pia walishiriki mihadhara kadhaa ambapo Ally Jamwaka alipata nafasi ya kufundisha kupiga tumba na Bitchuka alipata nafasi ya kurekodi wimbo mmoja na mganda Damascus Kafumbe (mwanafunzi wa Frank Gunderson) ambaye pia ni mkufunzi wa chuo hicho.

### MWAKA 2014

Kwa kutumia nembo ya 'Black Warrior' wanamuziki kadhaa walienda nchini Ujerumani ambako walialikwa kupiga nyimbo za Mlimani Park.

Wanamuziki hao ni Cosmas Chidumule, Hassan Rehani Bitchuka, Mafumu Bilal 'Bombenga', Joseph Kanuti, Tony Kalama, Juma Choka na Boniface Kachale.

Walishiriki tamasha la TFF lililokuwa linafanyika katika mji wa Rudolstadt kuanzia Julai 2 hadi Julai 6 mwaka 2014.

### MWAKA 2017

Mwishoni mwa mwaka 2017, bendi ilipata safari ya kwenda Kenya chini ya uratibu wa mwanamuziki Mtanzania Abbu Omar. Upande wa Kenya, safari iliandaliwa na mmiliki wa Deep West Resort pamoja na Citizen TV, ikishirikiana na mtangazaji (presenter) wao maarufu Mkongwe Uncle Fred Obachi Machoka.

Bendi ilipata nafasi ya kufanya maonyesho mawili katika siku 2 tofauti zote katika ukumbi wa Deep West Resort Club uliopo Nairobi, Kenya.

### WATUNZI BORA

Wanamuziki wafuatao ndio wanamuziki 6 wanaongoza kwa kutunga nyimbo nyingi zaidi (Zaidi ya nyimbo 10 kila mmoja) katika historia ya bendi; ambao ni Hassan Rehani Bitchuka (Nyimbo 30), Shaaban Dede (Nyimbo 27), Cosmas Thobias Chidumule (Nyimbo 16), Hussein Jumbe (Nyimbo 16), Max Bushoke (Nyimbo 11) na Joseph Mulenga (Nyimbo 10).

### UBINGWA WA MUZIKI WA DANSI NA TUZO MBALIMBALI

Bendi ya Mlimani Park Orchestra ndio bendi bora nchini Tanzania kihistoria. Bendi ilichukua ubingwa wa muziki nchini katika mashindano yaliyofanyika mwaka 1982. Katika michuano hiyo kwenye hatua ya nusu fainali bendi ya Mwenge Jazz 'Paselepa' iliishinda bendi ya JUWATA Jazz 'Msondo Ngoma' huku Bendi ya Mlimani Park Orchestra iliishinda bendi ya Arusha Jazz Band.

Kwenye fainali, bendi ya Mlimani Park Orchestra iliishinda bendi ya Mwenge Jazz . Sikinde walishinda kutokana na nyimbo 2 za "Tangazia Mataifa" na "Uhusiano wa Tanzania na Korea".

Bendi ilishinda mashindano ya MASHIBOTA (Mashindano Ya Bendi Za Muziki Wa Dansi Nchini) mwaka 1998 kutokana na wimbo wa "Mtoto wa Mitaani" uliotungwa na marehemu Hussein Jumbe.

Kwa muda wa miaka minne mfululizo (kuanzia mwaka 1984 hadi mwaka 1987) bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra nyimbo zake ziliongoza kwenye orodha ya nyimbo bora katika Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) hususan wimbo wake wa 'Neema' kutokana na idadi ya jinsi nyimbo zake zilivyokuwa zinaombwa na wasikiliza wa RTD katika vipindi vyake tofauti ikiwemo kipindi cha "Ombi Lako".

Bendi ya Mlimani Park Orchestra imeshinda baadhi ya tuzo za Kili Music Award ikiwemo ile ya mwaka 2009 ambapo bendi ilichukua tuzo ya Mtunzi Bora wa Muziki wa Dansi kutokana na wimbo wa 'Supu Umeitia Nazi' uliotungwa na mwanamuziki mwimbaji Karama Regesu.

Mwezi Novemba mwaka 2022, bendi ilipokea tuzo ya muziki ya heshima ya Afrika (Africa Honorary Music Award) kutoka taasisi iitwayo (The Music in Africa Foundation). Wasanii waliowahi kupokea tuzo hii kabla ya hapo ni Baaba Maal (Senegal, 2017), Eric Wainaina (Kenya, 2018), Ebo Taylor (Ghana, 2019), Bibie Brew (Ghana, 2019), Vusi Mahlasela (South Africa, 2021) na Thandiswa Mazwai (South Africa, 2021).


### IDADI YA NYIMBO NA ALBUM

Katika historia yake, bendi imeweza kutoa jumla ya albamu 32. Katika historia yake, bendi imeweza kutoa jumla ya nyimbo 216.

### IDADI YA WANAMUZIKI WALIOPITIA KWENYE BENDI

Idadi ya wanamuziki waliopitia katika bendi ya Mlimani Park Orchestra katika miaka 45 ni wanamuziki 98. Katika wanamuziki hao, wanamuziki 34 wametangulia mbele ya haki.

**Kwa ushauri na maoni; 0768 888 787 au 0784 122 020.**



Gama

Bitchuka

Benovilla

# Je, video ya mashambulizi ya Diddy itamwangamiza?







**LOS ANGELES, Marekani**

**PICHA** za video za CCTV zilithibitisha kile ambacho watu wengi katika tasnia ya muziki walijua kilikuwa kikisubiriwa; kipindi cha kuporomoka kwa wasanii wa hip-hop wenye ushawishi mkubwa katika historia.

Klipu za Sean "Diddy" Combs akimpiga teke mpenzi wake wa zamani Cassie Ventura akiwa amelala bila kusonga sakafuni, ziliimarisha kuanguka kwake, licha ya kuomba msamaha baada ya kuvuja.

"Sioni njia ya yeye kurudi kwenye umaarufu wa kimuziki baada ya tukio hili," alisema Amy DuBois Barnett, Mhariri mkuu wa zamani wa jarida la Ebony, ambaye ameandika kuhusu utamaduni wa hip-hop.

Sifa ya Combs katika tasnia hiyo "imeangaliwa kwa muda," aliongeza Barnett. "Watu wengi walifahamu hasira yake isiyozuilika."

Diddy ambaye awali alijulikana kama P Diddy, Puff Daddy au Puffy, ni mmoja wa wasanii maarufu zaidi na waliosifiwa zaidi wakati wote, akiwa na Tuzo tatu za Grammy na mamilioni ya mauzo ya rekodi kwa jina lake.

Kwa miaka mingi, hakuna chochote kilichoathiri kupanda kwa Diddy hadi alipopata hadhi kama msanii, mtayarishaji na mfanyabiashara. Kulikuwa na hadithi hasi katika tasnia hiyo, alisema Barnett, lakini nyingi zilikaa nje ya macho ya umma.

Novemba mwaka jana, Ventura alisuluhisha kesi dhidi ya Combs ambapo alimshutumu kwa ubakaji na ulanguzi wa kingono, kwa kiasi kisichojulikana. Lakini wakili wa Combs alisema suluhu hiyo; "kwa njia yoyote si kukiri makosa".

Watu mashuhuri waliendelea kumuunga mkono, lakini juhudi zao ziliisha pale video ya CCTV iliyopatikana na CNN ilipochapishwa hivi karibuni.

Shambulio lililoonyeshwa kwenye picha ni la kikatili. Baada ya kumpiga teke Ventura kama mpira wa miguu, Combs, akiwa amevaa taulo tu, anaonekana akimburuta kwenye sakafu.

Video hiyo inaonekana kuwa ni mkusanyiko wa picha za uchunguzi za tarehe 5 Machi 2016, ambazo CNN ilisema zilirekodiwa katika Hoteli ya InterContinental huko Century City, Los Angeles. Katika kesi yake, Ventura alikuwa ameeleza kisa cha Machi 2016 katika hoteli hiyo, ambapo Combs alidaiwa kumshambulia.

Msururu wa mashitaka mengine tangu wakati huo yaliletwa dhidi ya Combs kwa unyanyasaji, unyanyasaji wa kingono na ubakaji. Zilipowasilishwa, rapper huyo alizitaja tuhuma hizo kuwa "zinazochukiza" na kusema waathiriwa hao walikuwa wakitafuta "malipo ya haraka".

Lakini video ya kushambuliwa kwa Ventura ilidhoofisha juhudi zake za kukanusha kile kilichoonekana.

Combs alikuwa kimya kwa siku mbili baada ya kuachiliwa kwake, kabla ya kutuma ujumbe wa msamaha kwenye Instagram, akikiri kuwa kweli ni yeye aliyeonekana kwenye kanda hiyo na kuzitaja hatua zake kuwa "hazina madhara".

"Nilichukizwa wakati huo nilipofanya hivyo," alisema, "na nimechukizwa sasa."

"Nilienda na nikatafuta msaada wa kitaalamu," aliendelea. "Niliingia kwenye matibabu, kwenda kwenye kituo cha msaada wa kurekebisha tabia(rehab). Ilinibidi kumuomba Mungu huruma na neema yake. Samahani sana."

Combs hakumtaja Cassie Ventura katika msamaha wake, na wanasheria wake walimjibu, waakisema: "Kauli ya hivi karibuni ya Combs inamhusu



yeye mwenyewe kuliko watu wengi ambao amewaumiza."

Msamaha huo "ulichelewa sana," alisema Camron Dowlatshahi, wakili wa masuala ya burudani huko Los Angeles. "Inaonyesha kutoona mbali kwa Diddy, akidhani hatawajibishwa na kwamba ana pesa za kutosha kushughulikia kila kitu."

Barnett, ambaye ameandika kuhusu unyanyasaji wa wanawake katika tasinia ya rap, alielezea kauli hiyo kama "msamaha usioshauriwa zaidi kuwahi kutokea".

Alisema ulitoka kwenye "kitabu maarufu cha playman, kanusha, kanusha, kanusha . Ukipatikana na hatia . Omba msamaha, kisha zungumza kuhusu kwenda kutibiwa."

"Hakuna anayeuchukulia msamaha wake kwa uzito, hasa kwa sababu hapo awali alimshutumu Cassie na wengine kuwa watu waliotafuta mali. Hiyo ilikasirisha watu wengi katika tasnia ya muziki."

Ofisi ya Mwanasheria wa Wilaya ya Los Angeles ilisema Ijumaa kwamba haitaweza kuleta mashtaka kutokana na sheria ya vikwazo vya shambulio.

Je video ya CCTV, na uchunguzi unaoendelea, unaacha wapi kazi yake?

Katika muziki wake, Diddy mara nyingi amekuwa akitegemea ushirikiano na nyota wengine wa maarufu (A-list). Albamu yake ya mwisho ilishirikisha Mary J Blige, The Weekend, 21 Savage, John Legend. Kuna uwezekano mkubwa sana kwamba hawezi kuunda tena matoleo kama haya sasa.

Lakini iwa kutakuwa na athari kwa idadi kubwa ya wasikilizaji wake hilo si wazi. Kampuni ya Fitness Peloton imepiga marufuku muziki wake kwenye orodha za kucheza za mazoezi tayari, kulingana na TMZ, lakini kampuni zingine bado hazijatoa maoni.

# TFF ipewe maua yake kwa maendeleo ya soka



**Na Hamid Yassin**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), chini ya uongozi wa Rais wa Wallace Karia umethibitika kwa vitendo juu ya mustakabali wa kupigania mafanikio ya mpira wa miguu na utawala bora hapa Tanzania.

Haya hakuna haja ya kusimuliwa ili kuweza kuyafahamu bali kila mdau anajionea mwenyewe mambo makubwa yaliyofanywa na TFF hii katika kuhakikisha kandanda letu linazidi kukua.

Mizengwe, ujuaji mwingi wenyewe walikuwa wanaita 'Football Fitina', sasa inaelekea kwisha kama si kubaki stori tu kwenye soka letu tangu Karia na timu yake ya kina Wilfred Kidao waingie kwenye ofisi za pale Karume miaka kadhaa iliyopita.

Umefika wakati hakuna budi kuuupa hongera zao na kuwapigia makofi uongozi wa sasa Shirikisho hilo kwa namna wanavyopambana kuinua soka.

Hata kama kuna wadau wa soka wana ugomvi binafsi na viongozi wa TFF, basi wanaweza kuwasifu hata kinafikia. Kwani chini ya uongozi huu wa sasa ushindani kwenye Ligi Kuu ya NBC umeongezeka kwa kiasi kikubwa, na kupelekea kuongeza mvuto wa mashabiki wa ndani na nje ya nchi kuifuatilia ligi hiyo.

TFF hii imekuwa na mipango na mikakati kabambe ikiwemo kutafuta fedha ambazo zinafanya kila timu iwe imara na bora kutokana na fedha za wadhamini mbalimbali walioamua kuwekeza fedha zao baada ya kuona sasa mambo ni shwari kwenye soka letu.

Hata kufanya vizuri kwa vigogo vya soka nchini Simba na Yanga kwenye michuano ya kimataifa msimu uliopita pia kuna mkono wa TFF, kutokana na kuzipa ushirikiano mkubwa klabu hizo kongwe nchini.

Msimu uliopita wa CAF Champions League Tanzania ilikuwa ndio nchi pekee barani Afrika ambayo iliingiza timu mbili kwenye hatua ya robo fainali ya CAFCL, hii inachagizwa na ubora wa ligi, usimamizi mzuri wa viongozi wa soka lakini pia jitihada za TFF za kuendelea kutafuta wadhamini mbalimbali ili kuziongezea misuli ya kifedha timu za ligi kuu ya Tanzania.



**LIGI KUU YA VIJANA**

Msingi mzuri wa soka katika nchi yoyote duniani ni kusimamia vema kandanda la vijana, na katika hili uongozi wa Karia hauna duni kupongezwa kwani tumeshuhudia jitihada kubwa la kuendeleza soka la vijana.

Tanzania kwa sasa ipo ligi kuu kwa timu za vijana kwa maana ya U20 na U17 ligi ambazo awali hazikuwepo ila sasa TFF wameamua kutengeneza msingi kuanzia chini na kuibua vipaji vipya huku kubwa zaidi ni kuwepo na mwendelezo.

**LIGI YA WANAWAKE**

Tanzania ina ligi bora ya wanawake na ndio maana mara ya pili mfululizo bingwa wa CECAFA anatoka Ligi Kuu ya Tanzania, Msimu juzi ilienda Simba Queens kwenye mashindano ya CAF, msimu uliopita ilienda JKT Queens pengine na msimu ujao anaweza akaenda mwakilishi kutoka Tanzania.

Lakini pia Tanzania ni nchi ya pili ukiwatoa Afrika Kusini nchi zenye ligi daraja la Kwanza kwa wanawake Afrika tofauti na hapo nchi nyingine zote zina ligi kuu pekee, ndio maana pia tuna timu nzuri za taifa kwa soka la wanawake.

**TAIFA STARS**

Hapa napo si haba, tumeshuhudia timu yetu ya taifa ikishiriki fainali mbili za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON). Hii ni kwenye zile fainali zilizofanyika nchini Misri mwaka 2019 na zile za 2023 zilizofanyika mwaka huu kule Ivory Coast.

Kabla ya hapo timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, ilishiriki michuano hiyo mwaka 1980 kule nchini Nigeria wakati huo ikiitwa Kombe la Mataifa Huru ya Afrika.

Tukitoboa hapa na kuifanya timu yetu kuwa bora na kuweza kushindana na mataifa mengine, basi Tanzania huenda ikaenda kuliteka soko la mpira wa miguu Afrika.

**CAF YAIMWAGIA SIFA**

Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), nalo ni miongoni mwa taasisi kubwa zinazovutiwa na kasi ya maendeleo hapa nchini chini ya uongozi huu wa Karia.

Kauli hiyo ilitolewa na Rais wa Shirikisho hilo, Dk. Patrice Motsepe Agosti 13, mwaka 2021 alipokwenda kutembelea moja kati ya miradi mikubwa iliyokuwa inaanza kujengwa pale Kigamboni na kule Mnyanjani Tanga inayohusisha ujenzi wa vituo vya kuvumbua, kuibua na kukuza vipaji vya vijana kwenye mchezo wa mpira wa miguu kuanzia kwa vijana wadogo wenye umri chini ya miaka 9, 11, 13, 15, na kuendelea; mradi unasimamiwa na TFF wakiongezewa nguvu kubwa kutoka FIFA.

Rais Motsepe alisema kuwa, alifurahi na anajivunia kuona mambo makubwa na mazuri ya maendeleo kwenye mpira wa miguu yanayo fanywa na Rais Wallace Karia katika kuhakikisha soka linazidi kukua nchini na hata Afrika kwa ujumla.

Alipongeza pia utekelezaji mzuri wa majukumu kwa uongozi wa TFF akisema kuwa katika kila uongozi mzuri hapana shaka mafanikio lazima yawepo huku akisisitiza kulingana na utendaji huo mchezo wa mpira wa miguu wa Tanzania (Wanawake na Wanaume) utakuwa kwa kiwango kikubwa kwa Afrika na hata pengine kupiga hatua kubwa zaidi kuwa bora kwa ngazi ya Dunia.

Aidha, alimshukuru Katibu Mkuu wa CAF Veron Mosengo kwa kushirikiana bega kwa bega na uongozi wa TFF katika kulitimiza jambo hilo kwani amekuwa akishirikiana nao tangu likiwa wazo mpaka kufikia hatua ya kumalizika kwa miradi hiyo.

Haya ni mazuri machache tu kati ya mengi ambayo TFF hii ya Karia imelitendea haki soka letu katika kipindi chao chote cha uongozi mpaka sasa.

**Kwa maoni na ushauri; 0784 122 020, email; rassaultah@gmail.com**





# Wachezaji chipukizi wa kuangaliwa zaidi Ulaya

**Na Valensi Mbaga**

WAKATI mwingine ni dhahiri katika mpira wa miguu ni wachezaji gani wachanga wanapangwa kwa ukubwa. Lionel Messi ndiye mfano mmoja unaokuja akilini mara moja, ingawa kuna mingine mingi. Ilikuwa wazi kwamba Muargentina huyo alikuwa na uwezo wa kuwa mwanasoka wa kiwango cha dunia miaka michache tu baada ya kujiunga na Barcelona akiwa na umri wa miaka 13.

Vile vile, kuna vijana wachache wenye umri wa miaka 21 au chini ya miaka hiyo mpaka kufikia mwaka wa 2024 ambao wanaonekana kuwa na zana zote za kuwa wanasoka bora. Hatuna uwezekano wa kuona Messi mwingine akiibuka hivi karibuni, lakini hiyo haimaanishi kuwa hawatakuwa wachezaji bora kwa haki yao wenyewe.

Wafuataao ni wachezaji chipukizi watano bora zaidi katka soka la ulaya kwa sasa;

**5: ARDA GULER**

Linapokuja suala la kusajili vipaji vya vijana, ni wachache wanaofanya vizuri zaidi kuliko Real Madrid hivi sasa, kwa hivyo haikupaswa kushangaza kuona wababe hao wa Uhispania wakishinda mbio za kusaini talanta ya Kituruki Arda Guler katika msimu wa joto wa 2023.

Kiungo wa kati alikuwa akihusishwa sana na kila klabu kubwa za Ulaya kwa muda wa miezi 18 iliyopita, na ilikuwa tayari ni rahisi kuona sababu ya kumsajili kutokana na ubora wake.

Alipoibuka kutoka katika akademi ya Fenerbahce mnamo 2021, hadi mwisho wa kampeni ya 2021-22 alikuwa mfungaji bora zaidi wa kilabu huku akilinganishwa na mwenzake Mesut Ozil. Wengine walifikia hata kumbatiza jina la 'Messi wa Uturuki' kutokana na uwezo wake wa kuchezea chenga na jinsi Guler aliweza kupiga pasi hata akiwa kwenye maeneo magumu zaidi.

**4: MATHYS TEL**

Msimu wa Bayern Munich wa 2023-24 hakuwa bora kulingana na mpango. Lakini moja ya faida kubwa ya kuondoa kampeni kwenye Uwanja wa Allianz Arena imekuwa maendeleo ya Mathys Tel, ambaye anaendelea kutoa mchango wa kushinda mechi nyingi zaidi.

Mchezaji wa kati wakati wa miaka yake ya mapema katika akademi ya Rennes, Tel alianza kucheza katika safu ya ushambuliaji wakati wa ujana wake, na hajawahi kurudi nyuma.

Akiwa na umri wa miaka 16, alivunja rekodi ya Eduardo Camavinga ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kutokea katika klabu hiyo ya Ufaransa, na ingawa alicheza mechi saba pekee akiwa na Rennes, hiyo ilitosha kuwashawishi Bayern kuachana na 20m (£17m/$20m) ili kumpata na kwenda Ujerumani katika msimu wa joto wa 2022.

**3:WARREN ZAIRE-EMERY**

Hivi karibuni tutaishi katika ulimwengu ambapo Kylian Mbappe hachezi tena Paris Saint-Germain, na hivyo mabingwa hao wa Ufaransa watakuwa wakitafuta watu wenye vipawa ambao wanaweza kuwaongoza katika enzi mpya huko Parc des Princes.

Paris tayari wana kijana ambaye anaweza kuwa uso wa klabu kwa muongo ujao, ikiwa PSG wanataka hivyo.

Mabingwa hao wa Ufaransa hawana rekodi nzuri linapokuja suala la kuwapa wachezaji wa nyumbani nafasi ya kung'ara katika kiwango cha juu, lakini mara tu Zaire-Emery ilipoibuka na nguvu katika Ligi ya Vijana ya UEFA akiwa na umri wa miaka 15 mnamo 2021, alifuatiliwa kwa kasi kwenye kikosi cha kwanza.



Lamine Yamal

**2: ENDRICK**



Endrick

Tangu Neymar ajitokeze kutokea Santos, kwa sasa kumekuwa na kiwango cha msisimko unaomzunguka Endrick nchini Brazil, huku fowadi huyo akionekana kuwa supastaa anayesubiriwa baada ya kuibuka kwa kichwa chake cha habari katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Hakika Real Madrid wanakubaliana na dhana hiyo la sivyo hawangekubali kulipa kiasi cha Euro milioni 60 (£52m/$64m) katika mkataba wa Endrick mnamo Januari 2024.



Emery

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 hatakamilisha uhamisho wake kujiunga na Santiago Bernabeu hadi majira ya joto ya 2024, lakini msisimko miongoni mwa wana Madridista unaonekana, hasa baada ya kumtazama Endrick akimtimua Palmeiras kunyakua taji la Brazil mwishoni mwa 2023.

**1: LAMINE YAMAL**

Lamine Yamal anaweza kuwa na umri wa miaka 16 pekee, lakini ndani ya ukanda wa La Masia jina lake limekuwa liking'ara zaidi. Mazungumzo yamekuwa kwa muda mrefu kwamba akademi maarufu ya Barcelona ilifanya jambo ambalo lawezekana kupatikana kwa kupata mrithi anayestahili wa Lionel Messi.

Orodha ya rekodi ambayo Yamal tayari amevunja ni ya kushangaza mpaka sasa ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kuianza Barcelona, mfungaji mabao mwenye umri mdogo zaidi katika historia Barca na La mchezaji mwenye umri zaidi kuwahi mechi ya Ligi ya Mabingwa na mchezaji na mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya timu ya taifa ya Uhispania.



Masthystel



Arda Guler

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Juni 12 - 18, 2024 |

## Ufaransa, England zapigiwa upatu kutwaa Kombe la Ulaya

**BORN, Ujerumani**

MAANDALIZI yanaendelea kuelekea michuano ya Kombe la Mataifa ya Ulaya EURO 2024 itakayotifua vumbi kuanzia Juni 14 hapa Ujerumani huku timu za England, Ufaransa na wenyeji Ujerumani zikipigiwa upatu mkubwa kutwaa Kombe hilo.

Huku wenyeji Ujerumani wanakabiliwa na shinikizo la kupata matokeo bora katika mashindano hayo ya Euro 2024.

Hata hivyo, timu tatu ndio zinazopigiwa upatu kutawazwa mabingwa wa kandanda barani Ulaya nazo ni Ufaransa, Uingereza na wenyeji Ujerumani.



# Try Again ajiuzulu Simba

## ● Asema anampisha Mwekezaji MO
## ● Kuna wachezaji wanahujumu klabu



**Hamid Yassin**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba, Salumu Abdallah Mhene 'Try Again ' ameng'atuka katika nafasi hiyo kwa masilahi mapana ya Wekundu wa Msimbazi.

Try Again ametangaza uamuzi huo kupitia akaunti za klabu hiyo mitandaoni na kwenye baadhi ya vyombo vya habari huku akisisitiza amefanya uamuzi ili kuepusha shari ndani ya Simba.

"Kwa maslahi mapana ya Simba kwa kutambua mpira ni mchezo wa hisia, mimi kama Mwenyekiti wa Bodi nimemwomba Mwekezaji wetu Mohamed Dewji MO arejee kama Mwenyekiti wa Bodi nami nitasalia kama Mwanachama na kiongozi ambaye nipo tayari wakati wowote kuitumikia Simba, kwa maana hiyo natangaza kuondoka kwenye kiti"amenena Try Again.

Pia katika taarifa yake hiyo Try Again amesema kuwa, ndani ya klabu hiyo kuna wachezaji ambao ni wasaliti dhidi ya timu yao.

"Jambo lingine ni usaliti wa wachezaji, wachezaji tunawasajili kwa pesa nyingi tunalipa mishahara mikubwa lakini siyo waaminifu," amesema Try Again na kuongeza.

"Na niseme tu tunaendelea kuwachukulia hatua hawa wachezaji ambao siyo waaminifu".

Wiki iliyopita MO aliwataka wajumbe wote wa Bodi ya Wakurugenzi toka upande wake wajiuzulu ili aunde safu mpya ya uongozi na karibu wajumbe wote walitii amri hiyo isipokuwa Try Again ndiyo amechukua uamuzi huo jana.

Upande wa Wajumbe wa Bodi kutoka upande wa wanachama karibu wote wamesema wao hawatajiuzulu kwa sababu hawaoni sababu ya kufanya hivyo.



## Janabi: Simba, Yanga zinasajili bila kupima wachezaji


**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi amesema vilabu vikubwa vya Tanzania Simba, Yanga, Azam na vingine vinafanya usajili wa wachezaji kwa gharama kubwa kutoka nje na wa ndani lakini huwa havijui vyema hali za kiafya za wachezaji hao.

"Tungewashauri sana kabla hawajasaini mikataba, hebu naomba waje Hospitali ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila wafanyiwe check up. Maanake unamnunua mchezaji kwa dola laki moja, laki moja na nusu, dola laki mbili halafu anacheza mechi mbili baada ya hapo hachezi tena," amesihi Prof. Janabi na kuongeza.

"Sihitaji kutoa mifano, najua kuna moja ya klabu yetu kubwa imemsajili mchezaji mpaka leo hajacheza. Amecheza mechi mbili nafikiri kama sio tatu. Sasa tusiingie kwenye hizo gharama. Kitu cha kwanza nafikiri akishapatikana mchezaji aje apate vipimo, tunasema 'clean bill of health' kabla hamjatia saini ya mwisho," amesema Professa Janabi.

Profesa Janabi ameyasema hayo Juni 10, 2024 alipozungumza na vyombo vya habari katika Hospitali la Taifa ya Muhimbili-Mloganzila ambapo aliongozana na mmoja wa wagonjwa waliofanyiwa upandikizaji wa nyonga na magoti bandia katika Hospitali ya Mloganzila ambaye ni baba mzazi wa Haji Manara, Mzee Sunday Manara.





# Kombe la Kagame kutimua vumbi Julai

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) imetoa tarehe ya kuanza michuano ya Klabu Bingwa kwa timu za kanda hii (Kagame Cup) ambapo itaanza kutimua vumbi Julai 6 hadi 22 Dar es Salaam na Zanzibar huku watani wa jadi Simba na Yanga zote zikipangwa kushiriki.

Katika taarifa iliyotolewa jana na CECAFA kupita Mkurugenzi wake Mtendaji, John Auka Gecheo, imesema mbali na Simba na Yanga, pia zitakuwepo timu nyingine mbili toka Tanzania Bara za Azam FC na Coastal Uinon ya Tanga huku Zanzibar ikiwakilishwa na timu ya JKU SC.

Mbali ya timu hizo mwenyeji, CECAFA imesema kutakuwa na timu alikwa kutoka mataifa jirani ambazo tayari zimethibitisha kushiriki michuano hiyo ambazo ni TP Mazembe ya Congo DR, Nyasa Big Bullets ya Malawi na Red Arrows FC toka Zambia.

Gecheo amepasha kuwa, michuano hiyo ya Kombe la Kagame ilipangwa kuanza Julai 20 hadi Agosti 4 hapa Tanzania, lakini imerudishwa nyuma kupisha michuano mingine ya kimataifa kwa klabu ya msimu ujao 2024/2025.

Baraza hilo la Soka limesema michuano hiyo itazisaidia timu za ukanda huu wa Afrika Mashariki na kujiandaa na michuano mikubwa ya Klabu Bingwa na Kombe la Shirikisho Afrika na timu hizo toka Congo DR, Malawi na Zambai zitakuwa kipimo tosha kwa timu hizo kabla hazijashiriki mashindano hayo ya Afrika yanayotarajiwa kuanza mapema mwezi Agosti.

Pia Gecheo ametanabahisha kuwa, ile michuano ya Kombe la Challange kwa timu kubwa iliyopangwa kuanza Juni 29 hadi Julai 14 2024 imefutwa ili kutoa nafasi kwa timu zitakazoshiriki mashindano ya Kagame kujiandaa kikamilifu.

Timu nyingine zitakazoshiriki michuano ya Kombe la Kagame ni pamoja na Vital'o ya Burundi, APR FC ya Rwanda, El Merreikh, Al Hilal na Hai El Wadi za Sudan. Pia Gor Mahia FC (Kenya), SC Villa (Uganda) na El Merreikh Bentiu FC (Sudan Kusini).